BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT
1,018,116,895/-
KWA 1000/- TU!
SportPesa.CO.TZ | PIGA *150*87#



UKURASA 3

**Kinana** ashangaa wananchi kudaiwa mil. 920/- za deni la mwekezaji



UKURASA 21

**RONALDO ARUDI MANCHESTER**


# Nipashe

Jumatano Julai 27, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA

ISSN 0856 • Na. 0581019

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper


# MSIBA

**Ajali** yaua 13, wamo wanafunzi tisa, Samia atuma salamu za pole... *Endelea ukurasa 2*



Wananchi wakiangalia gari la shule binafsi ya awali na msingi King David, aina ya Toyota Hiace lenye namba za usajili T207CTS, lililopata ajali baada ya kutumbukia kwenye mtaro mkoani Mtwara jana na kusababisha vifo vya watu 13 na wengine 19 kujeruhiwa. **PICHA: BARAKA JAMALI**

## Serikali, TUCTA ngoma mbichi nyongeza mishahara

UKURASA 3



Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Prof. William Anangisye (katikati) na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Total Energies Tanzania, Jean Francois Scherp, wakionyesha nyaraka baada ya kutiliana saini mkataba, jijini Dar es Salaam jana, ambapo Total itatoa ufadhili wa mafunzo ya mafuta na gesi. Kushoto ni Mwanasheria Mkuu wa UDSM na Katibu wa Baraza la Chuo, Dk. Saudeen Mwakaje. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wamiliki wa mabasi wawekwa kikaangoni

UKURASA 2

MICHEZO SIMBA SC KARATA YA TATU MISRI LEO UK.24 | MAONI, KATUNI UK.6




Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (LATRA), Habibu Suluo, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma jana, kuhusu utekelezaji wa shughuli za mamlaka hiyo, ambapo kuanzia sasa mamlaka hiyo, imepiga marufuku biashara ndani ya magari ya abiria. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Msiba ajali iliyoua 13, wakiwamo wanafunzi 9

**Baraka Jamal na Abdallah Bakari,** MTWARA

NI msiba mkubwa uliopoteza maisha ya wanafunzi tisa, dereva, mfanyakazi wa shule na abiria mwingine na kusababisha majeruhi 17 kwenye ajali iliyotokana na basi la shule kutumbukia kwenye korongo.

Ajali hiyo ilitokea jana asubuhi wakati wanafunzi wa Shule ya Msingi King David iliyopo Manispaa ya Mtwara, Mikindani, wakielekea shuleni na miongoni mwao wakiwa wa familia moja.

Rais Samia Suluhu Hassan, ametuma salamu za rambirambi na pole kwa familia ya Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Brigedia Jenerali Marco Gaguti, kutokana na vifo hivyo.

Mzazi mmojawapo kati ya wanafunzi hao, Simon Chogwe, alisema watoto wake Johari Simon (8) wa darasa la tatu na Emmanuel Simon (5) wa darasa la awali, wamefariki dunia katika ajali hiyo.

Taarifa za awali zinaeleza kuwa gari hilo lilikuwa na wanafunzi wa shule nyingine ambao hadi sasa hawajafahamika majina na shule wanazotoka.

Chanzo cha ajali hiyo kinaelezwa kuwa ni gari hilo kufeli breki kwenye mteremko na kutumbukia kwenye korongo, katika eneo la Mjimwema, Kata ya Magengeni kuelekea Mitengo, Mikindani mkoani humo.

Katika ukurasa wake wa twiter Rais Samia aliandika: "Nimesikitishwa na vifo vya wanafunzi wanane wa Shule ya Msingi King David na watu wazima wawili vilivyotokea leo (jana) asubuhi huko Mtwara Mikindani, baada ya gari la shule kutumbukia shimoni, nawapa pole wafiwa, Mkuu wa mkoa na jamaa, Mwenyezi Mungu awarehemu marehemu na kuwaponya majeruhi."

Katika taarifa yake kwa umma, Rais alisema: "Nawapa pole majeruhi wa ajali hiyo na wafiwa wote na naungana na familia hizo katika kupindi hiki kigumu cha majonzi."

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mtwara, Nicodemas Katembo, akieleza kuhusu ajali hiyo, alisema ilitokea saa moja asubuhi, ikihusisha gari lenye namba za usajili T 207 CTS aina ya Hiace mali ya shule hiyo.

Alisema uchunguzi wa awali umebaini chanzo cha ajali hiyo ni kufeli kwa mfumo wa breki na kusababisha kutumbukia katika mtaro mkubwa.

"Ni kweli kumetokea ajali ya gari ya wanafunzi wa King David katika eneo la Mjimwema, tumewapoteza vijana wetu wanane, dereva na mtumishi mwingine wa shule hiyo, chanzo cha ajali ni hitilafu katika mfumo wa breki, gari likamshinda dereva likapoteza mwelekeo," alisema.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Dk. Hamadi Nyembea, alithibitisha kupokea miili kumi, majeruhi 19, lakini wanafunzi wawili walifariki wakati wakipatiwa matibabu na mtu mzima mmoja, huku wengine wakiendelea na matibabu, baadhi yao wako mahututi katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mtwara Ligula.

Nyembea alisema jana asubuhi, watano walikuwa wanapatiwa matibabu ya wagonjwa mahututi na mmoja alikuwa chumba cha upasuaji, wengine wenye majeraha walipatiwa huduma ya kushonwa.

"Asubuhi ya leo (jana) tumepokea majeruhi 19 na vifo 10 wanane wanafunzi na wawili ni watu wazima, kati ya hawa wanane, watoto wa kiume watatu, wasichana sita na watu wazima wawili, mwanaume na mwanamke, mmoja amefariki akipatiwa matibabu na wengine wana hali mbaya," alisema Mganga huyo.

Alitaja majina ya marehemu kuwa ni Johari (8), Emmanuel, Haji Ramadhani, Warda David, Humajla Changu, William Mrope, Christiano Jackson, Frida Maltoma na Precious Benjamin, wote ni wanafunzi.

Watu wazima ni Asha Salumu, Hassan Bakari na Shafii Hassan.

Jeshi la Polisi kwa kushirikina na hospitali hiyo wanaendelea na jitihada nyingine ili kuhakikisha usalama wa manusura wa ajali hiyo, Kamanda alisema.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi King David, Daniel Msilo, alisema kwa kawaida gari hilo linatakiwa kubeba wanafunzi 16, na ongezeko la abiria wengine linamuhusu dereva. "Gari yangu kwa kawaida inabeba watoto 16 tu ambao inawaleta shuleni, gari ya shule hairuhusiwi kubeba tofauti na wanafunzi wetu, ila inaonekana wengine walipewa lifti, kwa sasa tunafuatilia kujua ni wangapi kati hao 16 walikuwa wamepanda kabla ya ajali," alisema Msilo na kuongeza:

"Kwenye gari kulikuwa na wanafunzi wa shule zingine kama Mikindani...nimeambiwa kuwa kuna wanafunzi wangu watano wamefariki na majeruhi watatu, taarifa zaidi tutaitoa pindi tukikamilisha kukusanya taarifa sahihi," alisema.

Mkuu wa Mkoa, Brigedia Gaguti, aliagiza kukamatwa kwa wote waliosambaza picha zisizo na maadili mtandaoni za ajali hiyo, huku akitaka watu kuheshimu wengine.

## Wamiliki mabasi kikaangoni tiketi mtandao

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAMLAKA ya Udhibiti Usafiri Ardhini(LATRA), imesema baada ya Julai 31,mwaka huu, itachukua hatua dhidi ya wamiliki mabasi ya masafa marefu yatakayokuwa hayajaunganishwa na mfumo wa tiketi za kielektroniki.

Pia imesema mfumo maalum utakaomsaidia mwananchi kutambua mambo mbalimbali ikiwamo mwendo wa gari, utaanza kutumika Septemba, mwaka huu.

Vilevile, imepiga marufuku kufanya biashara, muziki mkubwa na mahubiri kwenye mabasi kwa kuwa imekuwa kero kwa abiria.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, Habibu Suluo, alisema hadi sasa mabasi 550 kati ya 7,502 yameunganishwa na mfumo wa tiketi mtandao na kwamba kwa siku yanakatisha wastani wa tiketi 5,000 hadi 7,000.

"Katika kikao cha tathmini tulichofanya kwa pamoja na LATRA, TRA (Mamlaka ya Mapato Tanzania) na TABOA (Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania), tumeazimia kwa pamoja kuwa kufikia mwisho wa mwezi huu, mabasi yote yawe yameunganishwa kwenye mfumo. Tutafanya tathmini nyingine kabla ya kuanza kulazimisha na kutoa adhabu,"alisema.

Alisema sheria inataka LATRA isitoe leseni kama basi halijafungwa mfumo.

"Ukija sasa hivi kuomba leseni huna mfumo wa tiketi za kielektroniki, hatukupi leseni, hii ina manufaa kwa mmiliki, serikali na abiria," alisema.

### KUDHIBITI MWENDO

Suluo alisema LATRA inaendelea kuboresha mfumo wa kufuatilia mwenendo wa magari (VTS) ambao utamwezesha mwananchi kupitia mfumo (APP) maalum itakayoanza kutumika Septemba, mwaka huu.

"Kupitia VTS tutakuwa na vituo vya taarifa kwenye stendi kuu za Dodoma na Dar es Salaam ambapo abiria watakuwa na uwezo wa kutambua mahali mabasi wanayosubiri yalipo," alisema.

Hata hivyo, alisema kwa sasa VTS imeunganishwa kwenye mabasi 7,502 na vichwa vya treni 26.

"Tunajua kuna watu wanahujumu mfumo tutafanya uchunguzi tujue tatizo liko wapi kwa kushirikiana na mamlaka zinazohusika. Tutaangalia kwa nini magari yanakwenda mwendo kasi wakati yamefungwa VTS. Ziko teknolojia nyingi tutafuatilia," alisema.

Alisema basi lisilo na VTS ni kosa kisheria na yaliyofungwa ndio yanayotambuliwa na mamlaka hiyo.

Pia alisema wamepokea maombi kutoka shirika la reli kudhibiti mfumo wa mafuta ili waone mafuta yao yanavyotumika.

### MARUFUKU

Alisema ikitokea madhara kutokana na biashara iliyofanywa kwenye basi ni kitu ambacho sio mahali pake, biashara kwenye mabasi marufuku, wale wa kutoa mahubiri kwenye mabasi marufuku ni kwa mujibu wa matakwa ya kanuni, sasa ukikuta kwenye mabasi inafanyika hivi ni kosa.

Pia alisema kumekuwapo na ongezeko la vyombo vya usafiri kila mwaka ambapo kwa mwaka 2021/22, idadi ya mabasi ya abiria yaliyopata leseni ni 47,547 na magari ya mizigo ni 143,011.

## HABARI KITAIFA

# Kinana ashangazwa, wananchi kudaiwa mamilioni ya mwekezaji

**Na Beatrice Shayo, aliyekuwa** KATAVI

SAKATA la mgogoro wa ardhi mkoani Katavi limemshangaza

Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tanzania Bara, Abdulrahman Kinana, ameelezea kushangazwa na mgogoro wa ardhi Katavi baada ya kupewa taarifa kwamba wananchi wanadaiwa Sh. milioni 918 na serikali, licha ya kutapeliwa na mwekezaji aliyetoweka na kuwaachia deni hilo.

Kutokana na hali hiyo, amezuia shughuli zote za upimaji katika eneo hilo lenye ekari 500 hadi mgogoro huo utakapopatiwa ufumbuzi na serikali.

Kinana alipatwa na butwaa wakati akiwasikiliza wananchi hao ambao ardhi yao ilichukuliwa na mwekezaji kwa miaka 12 hadi sasa ambaye alidai anajenga Taasisi ya Chuo Kikuu cha Kilimo Katavi (KUA) bila kuwalipa fidia.

Mwekezaji huyo amechukua kiwanja namba moja na mbili kitalu A vyenye ukubwa wa ekari 500 eneo la Kazima, Manispaa ya Mpanda kwa kukopa Benki ya KCB Sh. milioni 600 kwa kutumia hati ya wananchi hao, kwa ajili ya ujenzi wa chuo lakini ameingia mitini na wananchi kuendelea kuteseka.

Akizungumzia mgogoro huo, Ofisa Ardhi Manispaa ya Mpanda, Brian Severe, alisema baada ya kupima viwanja hivyo taasisi hiyo ambayo inajulikana kwa jina la KUA ilikaa na viwanja hivyo kwa muda mrefu.

"Bahati mbaya wakati wanachukua haya maeneo hawakulipa fidia wakaingia kwenye mgogoro baina ya wananchi na halmashauri kuhusu kuchukua maeneo bila kuwalipa fidia, halmashauri ilitatua mgogoro huu kwa kushirikiana na uongozi wa ngazi ya wilaya na mkoa," alisema Severe.

Baada ya kusikiliza maelezo hayo Kinana alihoji aliyekopa ni nani na kujulishwa aliyekopa ni taasisi inayoitwa KUA.

"Hizo hati zilikuwa zimewekwa Benki ya KCB kama dhamana baada ya serikali kufuatilia zile hati zilirudishwa Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda,"alisema Severe.

Kinana alimtaka Mkurugenzi wa Mpanda, Sophia Kumbuli, kuelezea kama ni kweli hati hizo zilirudishwa au la.

Alisema kwa taarifa aliyo nayo zimerudishwa kwa vile maeneo yamerudishwa kwa wananchi na inadaiwa Shilingi zaidi ya milioni 800 na wao kama Manispaa ya Mpanda hawataweza kulipa deni hilo kwa kuwa watashindwa kutoa huduma katika maeneo mengine.

Baada ya kusikiliza maelezo hayo Kinana alihoji: "Nani aliyekwenda benki kukopa nijibuni maana wananchi wanataka haki yao ama muwalipe fedha zao hakuna njia ya mkato hiyo taasisi ni nani aliyekwenda kukopa hao wawekezaji ni kina nani hawana majina, hawana kampuni hawajulikani wanaitwaje je, wako wapi?"

"Huu ni utapeli tu, wizi na ufisadi hawa wananchi wana ardhi yao wamekuja matapeli hii nchi imejaa matapeli wengi... mtu anasema anataka kuanzisha chuo kikuu halafu anayeanzisha chuo kikuu anakuja kukopa hela benki. Hivi unaweza kuanzisha ujenzi wa chuo kikuu kwa Sh. milioni 600? Chuo kikuu kinaanza na mambo makubwa," alisema.

# Serikali na TUCTA ngoma mbichi nyongeza mishahara

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema bado inaendelea na majadiliano na viongozi wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA) kuhusu malalamiko ya nyongeza za mishahara.

Hata hivyo, viongozi wa TUCTA wamesema leo watawasilisha hoja zao kwa maandishi serikalini na hawataondoka Dodoma hadi kujua hatma ya hoja hiyo.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, alisema serikali imeanza majadiliano na awali na shirikisho hilo ambayo yamehudhuriwa na viongozi mbalimbali akiwamo Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama.

"Julai 22, mwaka huu serikali iliahidi kutoa ufafanuzi juu ya hoja iliyozungumzwa na wafanyakazi kuhusu nyongeza za mshahara ya kima cha chini iliyotokea kwenye mishahara ya Julai. Tuliahidi leo (jana) kukutana na TUCTA kuwasikiliza. Napenda kuwajulisha tumekutana leo (jana)."

"Tumekutana na viongozi wa TUCTA na viongozi kwenye vyama vya wafanyakazi na baada ya mazungumzo ya awali ya leo (jana), viongozi wameomba muda wakajadiliane na baadaye kuzungumza na serikali. Nawajulisha kwamba mazungumzo yameanza na viongozi wa TUCTA watakapokamilisha mazungumzo yao, watakuja kukutana na serikali ili tusikilize hoja zao na baada ya hapo tutatoa tamko," alisema.

Alipoulizwa kuhusu muda, alisema wamewapa nafasi hadi pale watakapokamilisha majadiliano yao na kuwasilisha serikalini.

**KAULI YA TUCTA**

Wakati Msigwa akisema hayo, Rais wa TUCTA, Tumaini Nyamhokya, alisema viongozi wa serikali wamefika na wamezungumza na wamewaonyesha kiwango gani watumishi na viongozi wao ambavyo hawajaridhika na utaratibu wa nyongeza ya mshahara ulivyofanyika.

"Kwa hiyo tumewakabidhi wenzetu wa serikali na sisi tupo hapa Dodoma, tunaendelea na majadiliano hadi tupate majibu. Kwa leo (jana) tumeonesha kitu ambacho hatukukitegemea, tulitarajia hiyo nyongeza aliyoitaja Rais ya asilimia 23.3 itawagusa wafanyakazi wenye vima vyote kwa kiwango kilichozoeleka," alisema katika Ofisi za Chama cha Walimu Tanzania (CWT) akiwa ameambatana na viongozi waandamizi wa shirikisho hilo.

"Kwa bahati mbaya kiwango kimekuwa cha chini na kimeumiza sana wafanyakazi. Tumeendelea na mazungumzo na serikali na tumefikia hatua hiyo na tunaendelea na mjadala. Tumezungumza hadi jioni hii tutaweka kimaandishi na tutakabidhi kesho (leo). Baada ya hapo tutaangalia kitu gani kinafanyika," aliongeza.

Nyamhokya alisema kuna maoni yao tayari wamewasilisha serikalini na leo watawasilisha mengine kimaandishi ili kufanyiwa kazi kiofisi.

"Kwa bahati mbaya kilichotokea kwenye 'salary slip' zao kimekuwa tofauti na matarajio yao na sisi tumeleta kilio kwa serikali. Bahati nzuri wamepokea na wanalifanyia kazi," alisema.


**TOL Gases Limited** We Deliver

Plot 4B, Nyerere Road, P.O Box 911, Dar es Salaam
Telephone: +255 22 2860047/9, Fax: 2 8 64041, E-mail: info@tolgases.co.tz

## NOTICE
## 2021 ANNUAL GENERAL MEETING

**NOTICE IS HEREBY GIVEN THAT** the Meeting of the Shareholders of TOL Gases Limited for the year ended December, 31, 2021 will be held on a hybrid of physical attendance at the Julius Nyerere International Convention Centre (JNICC) and via ZOOM video conferencing on 19th August, 2022 at 9.00 am to transact the following business:-

1. Adoption of the Agenda.
2. Confirmation of Minutes of the year 2020 Annual General Meeting held on 27th August, 2021.
3. Matters arising from minutes of the year 2020 Annual General Meeting.
4. Chairman's Statement.
5. To receive the Directors' Report, Auditors' Report and the Audited Financial Statements for the year ended December 31, 2021.
6. To approve Dividend Payment.
7. To approve Directors' Fees.
8. To appoint Auditors for the year 2022.
9. Amendment of MEMARTS
10. Any other business (duly notified at least seven days before the meeting)

Registration for participating in the ZOOM Video Conferencing should be done through phone no **0685750201/0685750203.**

A member entitled to attend and vote at the Meeting is entitled to appoint any person (whether a member of the Company or not) to attend and vote in his stead.

All proxy forms or letters appointing proxy must be lodged at the office of the Company Secretary at least 48 hours before the time fixed for the holding of the meeting or via email to **mjuliana@tol-gases.co.tz /nlulu@tol.gases.co.tz**

**BY ORDER OF THE BOARD**

**CORNELIUS KASIYA KARIWA**
**COMPANY SECRETARY**

216960702

Directors: M.N.Shirima – Chairman(Tanzanian), S. Mponji – (Tanzanian), J.Massawe – (Tanzanian), S.Selestine – TR – URT (Tanzanian), Prof.ATemu – (Tanzanian), Eng. J. Machange – (Tanzanian)



FSSP Field Support Services Project | Tanzania

## CONSULTANCY POSITION
## DESIGN EXPERT AND /OR PRINTER FOR MAPPING GAC PROJECTS

PricewaterhouseCoopers Limited (PwC), on behalf of our client, invites eligible Design Expert and /or Printer to indicate their interest to provide consultancy services to the Field Support Services Project (FSSP) Tanzania, to map projects funded by the Global Affairs Canada (GAC).

The Design Expert will use location (town) data to create a virtual map compatible with Microsoft Office software, Adobe software, or Google Maps, from which, a print version can be created.

The ideal Design Expert and /or Printer will possess the following key qualifications:

- Knowledge about the technical aspects of geographical data management and utilization
- Proficiency with software for development of virtual map compatible with Microsoft Office software, Adobe software, or Google Maps,
- Knowledge about data processing, storage, usage of geographic data and visualization
- Good interpersonal communication and coordination skills
- Ability to adhere to deadlines and flexibility.

Interested individual Design Expert and /or Printer may obtain detailed description of these services by sending a request email to **procurement@fssptz.org**. Requests for further information will be received up to two (2) working days prior to the submission deadline. Any request received later than that may not be responded to.

Expressions of Interest should be sent ONLY electronically to **procurement@fssptz.org** not later than **31st July 2022 at 23:59 hours.** Late Expressions of Interest shall not be accepted for evaluation, irrespective of the circumstances.

**FSSP Manager**

216957601

Tanzania Commercial Bank
Growing stronger together

www.tcbbank.co.tz

# UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA(HESABU AMBAZO HAZIJAKAGULIWA)

Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

# TANZANIA COMMERCIAL BANK PLC

## WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 JUNI, 2022

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | | | Robo Mwaka /Mwaka wa sasa 30.06.2022 | Robo Mwaka/Mwaka uliopita 31.03.2022 |
|---|---|---|---|---|
| A. | | MALI | | |
| | 1 | Fedha Taslimu | 62,114 | 47,576 |
| | 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 48,661 | 46,526 |
| | 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 105,096 | 104,766 |
| | 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 84,817 | 69,805 |
| | 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 253 | 423 |
| | 6 | Miamala Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| | 7 | Bili Zilizoafikiwa | 0 | 0 |
| | 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | 0 | 0 |
| | 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 145,384 | 139,037 |
| | 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | 0 | 0 |
| | 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 770,613 | 732,994 |
| | 12 | Mali Nyingine | 46,371 | 49,040 |
| | 13 | Uwekezaji wa Hisa | 0 | 0 |
| | 14 | Akaunti za udhamini | 0 | 0 |
| | 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 20,999 | 21,412 |
| | **16** | **JUMLA YA MALI** | **1,284,309** | **1,211,580** |
| B | | DHIMA | | |
| | 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 0 | 0 |
| | 18 | Amana za Wateja | 835,519 | 768,387 |
| | 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 |
| | 20 | Amana Maalumu | 172,704 | 169,724 |
| | 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 3,618 | 4,997 |
| | 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | -0 | -0 |
| | 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 20,896 | 19,420 |
| | 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | 0 | 0 |
| | 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| | 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 2,504 | 2,365 |
| | 27 | Dhima Nyingine | 25,438 | 28,169 |
| | 28 | Madeni | 106,945 | 103,672 |
| | **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **1,167,625** | **1,096,734** |
| | **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI** ***(16 kutoa 29)*** | **116,684** | **114,845** |
| C. | | FEDHA ZA WANAHISA | | |
| | 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 28,072 | 28,072 |
| | 32 | Akiba ya Mtaji | 0 | 0 |
| | 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 73,955 | 75,200 |
| | 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 3,719 | 1,880 |
| | 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 10,939 | 9,694 |
| | 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | 0 | 0 |
| | **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **116,684** | **114,845** |
| | 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 207,546 | 195,905 |
| | 39 | Mikopo Chechefu | 72,052 | 81,111 |
| | 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 11,275 | 14,848 |
| | 41 | Mali Nyingine Chechefu | 945 | 11 |
| D. | | BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA | | |
| | (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 9.09% | 9.48% |
| | (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 9.15% | 10.77% |
| | (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 78.12% | 80.27% |
| | (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 60.00% | 60.50% |
| | (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 79.51% | 80.62% |
| | (vi) | Ongezeko la Amana | 7.47% | 3.30% |
| | (vii) | Ongezeko la Mali | 6.00% | 2.28% |

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2022

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Robo ya Mwaka sasa | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) | Limbikizo la Mwaka wa sasa | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) |
|---|---|---|---|---|
| | 30-Jun-22 | 30-Jun-21 | 30-Jun-22 | 30-Jun-21 |
| 1 Mapato ya Riba | 34,631 | 33,297 | 69,353 | 65,355 |
| 2 Gharama za Riba | (11,971) | (9,716) | (22,575) | (19,246) |
| 3 Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2) | **22,660** | **23,580** | **46,778** | **46,110** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | (40) | 1,533 | (55) | (85) |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (3,433) | (3,393) | (6,914) | (6,941) |
| 6 **Mapato Yasiyo ya Riba**: | **8,311** | **9,622** | **16,215** | **18,512** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 1,199 | 1,428 | 2,622 | 2,587 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 4,732 | 4,150 | 8,871 | 8,714 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | 2,381 | 4,044 | 4,722 | 7,211 |
| 7 **Gharama Zisizo za Riba:** | **(24,138)** | **(23,823)** | **(48,811)** | **(45,560)** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 12,146 | 11,216 | 24,492 | 22,458 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | 1,819 | 1,235 | 3,373 | 2,422 |
| 7.3 Gharama Nyingine | 10,174 | 11,372 | 20,946 | 20,679 |
| 8 **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **3,360** | **7,520** | **7,212** | **12,036** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | 1,521 | 2,552 | 3,493 | 4,502 |
| 10 **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **1,839** | **4,968** | **3,719** | **7,534** |
| 11 **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - | - | - |
| 12 **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **1,839** | **4,968** | **3,719** | **7,534** |
| 13 Idadi ya Waajiriwa | 1,093 | 1,060 | 1,093 | 1,060 |
| 14 Mapato kwa Hisa | 66 | 177 | 132 | 268 |
| 15 **Idadi ya Matawi** | 48 | 42 | 48 | 42 |
| BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI | | | | |
| (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.15% | 0.44% | 0.31% | 0.89% |
| (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 1.58% | 4.59% | 3.21% | 7.02% |
| (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 56.21% | 55.51% | 57.04% | 54.32% |
| (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 2.25% | 2.73% | 4.71% | 5.48% |

Tarakimu za wastani zitakokotolewa kwa kujumlisha salio la mwisho kwa miezi inayohusika katika kipindi na kugawanya kwa idadi ya miezi katika kipindi hicho.

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 30 JUNI, 2022

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Robo Mwaka ya sasa 30-Jun-22 | Robo Mwaka iliyopita 31-Mar-22 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Jun-22 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Jun-21 |
|---|---|---|---|---|
| **I: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | 3,360 | 3,853 | 7,212 | 12,036 |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | |
| - Hasara Katika Mali | 5,964 | 5,939 | 12,201 | 11,601 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (41,898) | (14,394) | (56,292) | (40,948) |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 70,112 | 29,996 | 100,108 | 175,770 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (2,102) | (2,611) | (11,183) | (25,290) |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 2,669 | (4,133) | (7,465) | (30,679) |
| - Kodi Iliyolipwa | (1,521) | (1,973) | (3,493) | (4,502) |
| - Mengineyo (bainisha) | (21,901) | 19,362 | (23,627) | (38,587) |
| ***Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji*** | **14,684** | **36,040** | **17,461** | **59,402** |
| **II: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za** | | | | |
| Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (933) | (980) | (1,914) | (3,463) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa | - | - | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | **(933)** | **(980)** | **(1,914)** | **(3,463)** |
| **III: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | (1,000) | (1,798) | (2,798) | (2,738) |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | ***(1,000)*** | ***(1,798)*** | ***(2,798)*** | ***(2,738)*** |
| **IV: Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | 12,750 | 33,261 | 12,749 | 53,201 |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | **144,937** | **111,676** | **144,937** | **120,526** |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 157,687 | 144,937 | 157,687 | 173,727 |

## TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2022

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | 28,072 | - | 75,447 | (0) | 0 | 9,694 | 113,213 |
| Mabadiliko ya mpito ya IFRS 9 | - | - | - | | | | - |
| Hamisho kwenda hifadhi ya kisheria | - | - | (1,493) | 1,245 | - | | (248) |
| Faida ya mwaka | - | - | - | - | - | 3,719 | 3,719 |
| Mapato mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| Hifadhi ya jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Hamisho kwenda/kutoka mapato yaliyohifadhiwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | 28,072 | - | 73,955 | 1,245 | 0 | 13,413 | 116,684 |
| **Mwaka uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | 28,072 | - | 66,533 | (0) | 0 | 9,694 | 104,299 |
| Hamisho kutoka hifadhi ya udhibiti | - | - | - | - | - | - | - |
| Faida ya mwaka | - | - | 9,167 | - | - | - | 9,167 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | (253) | - | - | - | (253) |
| Hisa za ziada | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la ziada ya jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Hasara ya sasa ya manufaa yaliyofafanuliwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Kurudishiwa Gawio lililosimamishwa | | | - | | | | - |
| Mengeineyo | | | | | | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | 28,072 | - | 75,447 | (0) | 0 | 9,694 | 113,213 |

## BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 JUNI, 2022

Benki ililipa faini ya shilingi Laki 1, Milioni 1.00 na million 69 kutokana na upungufu wa fedha zilizopelekwa Benki kuu(Bot counter shortage), kuchelewa kuwasilisha taarifa ya Ukwasi( Liquidity),kuchelewa kuwasilisha taarifa ya robo mwaka na mpango kazi wa ukaguzi wa ndani mwaka 2022.

Katika kuandaa taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8)

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| **SABASABA K. MOSHINGI** (Ofisa Mtendaji Mkuu) | **Imesainiwa** | **20.07.2022** |
| **MS. REGINA E. SEMAKAFU** (Mkuu wa Fedha) | **Imesainiwa** | **20.07.2022** |
| **SOSTHENES F. NYENYEMBE** (Mkaguzi Mkuu wa Ndani) | **Imesainiwa** | **20.07.2022** |

Sisi tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi,tunathibitisha usahihi wa Taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathimini taarifa hizi,na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya kimataifa vya uwasilishaji wa Taarifa za fedha na matakwa ya sheria ya Benki na Taasisi za fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi

| | | |
|---|---|---|
| **DR. EDMUND B. MNDOLWA** Mwenyekiti wa Bodi | **Imesainiwa** | **20.07.2022** |
| **MS. ANNE C. MBUGHUNI** Mjumbe wa Bodi | **Imesainiwa** | **20.07.2022** |

tcbbank

Head Office, Millenium Tower II, 10th Floor, Kijitonyama Opp. Makumbusho Village,
P.O. Box 9300, Dar Es Salaam | Telephone; +255 22 216 2940
E-mail: info@tcbbank.co.tz | www.tcbbank.co.tz | Customer Care: +255 787 669977 | +255 788 767 683 | +255 658 767 683

216959401

# TANGAZO


**Tanzania Commercial Bank** — Growing stronger together

# MINIMUM DISCLOSURE OF RATES AND CHARGES 2022

*All charges are VAT exclusive.

| PRODUCT | MINIMUM OPENING BALANCE | | MONTHLY MAINTANCE FEES | | MINIMUM OPERATING BALANCE | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | TZS | USD | TZS | USD | TZS | USD |
| Call account | 100,000.00 | 100.00 | 10,000.00 | 5.00 | 100,000.00 | 100.00 |
| Business Current Account | 100,000.00 | 100.00 | 20,000.00 | 20.00 | 100,000.00 | 100.00 |
| Personal current Account | 100,000.00 | 100.00 | 7,000.00 | 5.00 | 50,000.00 | 100.00 |
| Vikundi Current Account | 100,000.00 | N/A | FREE | N/A | 50,000.00 | N/A |
| Quick Account | 20,000.00 | 10.00 | 1,800.00 | 0.86 | 20,000.00 | 10.00 |
| Salary Account | FREE | N/A | 1,800.00 | N/A | 0 | N/A |
| Tabasamu Individual | 10,000.00 | N/A | FREE | N/A | 10,000.00 | N/A |
| Tabasamu Group Account | 50,000.00 | N/A | FREE | FREE | 50,000.00 | N/A |
| Platinum Account | 15,000.00 | N/A | 1,800.00 | N/A | 15,000 | N/A |
| Minor Account | 20,000.00 | N/A | FREE | N/A | 20,000 | N/A |
| Group Account | FREE | N/A | FREE | N/A | 0 | N/A |
| Scout Minor Account | 10,000.00 | N/A | FREE | N/A | 10,000 | N/A |
| Scout Account | 30,000.00 | N/A | FREE | N/A | 30,000 | N/A |
| Wavuvi Account | 10,000.00 | N/A | 1,800.00 | N/A | 10,000 | N/A |
| Wadu Account | 20,000.00 | N/A | FREE | FREE | 20,000 | N/A |
| Kivulini Account | FREE | N/A | 700.00 | N/A | 1,500.00 | N/A |

### CASH SERVICES

| DESCRIPTION | BANDS | CHARGES |
|---|---|---|
| Cash deposit | | FREE |
| | Withdrawal below 400,000 | 1,800.00 |
| | Withdrawal 400,001 - 800,000 | 3,000.00 |
| | Withdrawal from 800,001 - 1,200,000 | 4,400.00 |
| | Withdrawal from 1,200,001 - 10,000,000 | 5,000.00 |
| | Withdrawal from 10,000,001 - 50,000,000 | 6,000.00 |
| | Withdrawal from 50,000,001 -100,000,000 | 14,000.00 |
| Cash withdrawal TZS | Withdrawal from above 100,000,000 | 0.12% max 170,000 |
| | Withdrawal below 50 | 1.00 |
| | Withdrawal from 51-1,000 | 2.50 |
| | Withdrawal from 1,000 -2,250 | 5.00 |
| | Withdrawal from 2,251-5,000 | 15.00 |
| Cash withdrawal USD | Withdrawal Above 5,000 | 0.25% |
| **BANK STATEMENT** | **TZS** | **USD** |
| Balance enquiry over the counter | 1000.00 | USD equivalent |
| Statement per page | 2,000.00 | USD equivalent |
| **CHEQUE SERVICE** | **TZS** | **USD** |
| Cheque book per leaf | 500.00 | USD equivalent |
| Cheque clearing | FREE | FREE |
| Unpaid cheque/insufficient fund | 150,000.00 | USD equivalent |
| Stop Payment order | 30,000.00per leaf Max 300,000.00 | USD equivalent |

| DORMANT ACCOUNT | | |
|---|---|---|
| Dormant account fee | FREE | |
| Re-activation | FREE | |

| ACCOUNT CLOSURE | TZS | USD |
|---|---|---|
| Closing account fee | 13,000.00 | USD equivalent |

| OTHER SERVICES | TZS | USD |
|---|---|---|
| Government Securities transaction Handling fees | 50,000.00 | N/A |
| Confirmation to Auditors | 45,000.00 | USD equivalent |
| Introduction letter/Confirmation to Embassies | 45,000.00 | USD equivalent |

| FUND TRANSFER SERVICE | TZS | USD |
|---|---|---|
| TISS-Outward | 10,000.00 | USD Equivalent |
| TISS-Inward | FREE | FREE |
| EFT-Outward | 2,000.00 | N/A |
| EFT-Inhouse | 1,500.00 | N/A |
| TT-Outward | N/A | 55 |
| TT-Inward | N/A | 5 |
| Internal Transfer | FREE | FREE |
| Standing Order - Within the Bank | FREE | FREE |
| Standing Order - To other Bank | 13,000.00 | USD Equivalent |
| Salary Handling-Cheque list | 1,000.00 | USD Equivalent |

### AGENT BANKING SERVICE

| DESCRIPTION | BANDS | CHARGES |
|---|---|---|
| Deposit | PER TRANSACTION | FREE |
| Withdrawal | 0.01 - 10,000.00 | 800.00 |
| | 10,000.01 - 20,000.00 | 1,250.00 |
| | 20,000.01 - 50,000.00 | 1,500.00 |
| | 50,000.01 - 100,000.00 | 2,250.00 |
| | 100,000.01 - 200,000.00 | 2,750.00 |
| | 200,000.01 - 300,000.00 | 4,200.00 |
| | 300,000.01 - 400,000.00 | 5,500.00 |
| | 400,000.01 - 500,000.00 | 6,000.00 |
| | 500,000.01 - 700,000.00 | 6,500.00 |
| | 700,000.01 - 1,000,000.00 | 7,500.00 |
| | 1,000,000.01 - 1,500,000.00 | 8,500.00 |
| | 1,500,000.01 - 2,000,000.00 | 9,000.00 |
| | 2,000,000.01 - 3,000, 000.00 | 10,000.00 |
| Balance Enquiry | | 100.00 |
| Mini Bank Statement | | 200.00 |

### POPOTE ATM SERVICE

| DESCRIPTION | CHARGES |
|---|---|
| Popote ATM card Issuance/Replacement | 15,000.00 |
| PIN Re-issue | 1000.00 |
| Collection of ATM Card at non-Domicile Branch | 6,500.00 |
| Uncollected and Destroyed ATM Card | 5000.00 |
| Balance Enquiry | 300.00 |
| TCB ATM Withdrawal | 1,300.00 |
| Withdrawal to Other Bank Umoja Switch ATMs | 1,300.00 |
| Card Maintenance | 5000.00 |

### POPOTE VISA CARD

| DESCRIPTION | CHARGES |
|---|---|
| Popote VISA issuance/Replacement | 20,000.00 |
| ATM Withdrawal - Domestic | 3,350.00 |
| Balance Inquiry - Domestic | 1,000.00 |
| ATM Withdrawal - International | 5,500.00 |
| Balance Inquiry - International | 2,000.00 |

### POPOTE MOBILE BANKING / INTERNET BANKING

| DESCRIPTION | BANDS | CHARGES |
|---|---|---|
| Registration | | FREE |
| | 500 -10,000.00 | 850.00 |
| | 10,000.01 - 50,000.00 | 1,200.00 |
| | 50,000.01 - 100,000.00 | 1,500.00 |
| | 100,000.01 - 250,000.00 | 2,800.00 |
| | 250,000.01 - 500,000.00 | 4,600.00 |
| | 500,000.01 - 750,000.00 | 7,500.00 |
| Transfer Bank to MNO | 750,000.01 - 1,000,000.00 | 10,000.00 |
| From MNO to Bank (Deposit) | | FREE |

| LETTER OF CREDIT ISSUED (IMPORT LCS) | CHARGES |
|---|---|
| Charges on Draft LC | USD 60 |
| LC commission per quarter | 1% per quarter or part thereof. Min USD 150 or foreign eqv |
| LC commission per quarter with cash cover | 1% per quarter or part thereof. Min USD 150 or foreign eqv |
| Amendment fee per quarter on the tenor extended or amount increased | 1% perquarter Min USD 150 or foreign eqv |
| Other amendments | USD equiv 60 or foreign eqv |
| Discrepancy fee per pack | USD equiv 60 or foreign eqv |
| Documen examination Fee per pack | 0 |
| Cancellation charges | USD 60 or foreign eqv. |
| Swift charges | USD 60 or foreign eqv. |
| Non-Payment of Bills Due Date | 0 |
| Expire unutlised Letters of Credit | 0 |

### LENDING INTEREST RATES AND OTHER CHARGES

| LOANS | CATEGORY | INTEREST RATE |
|---|---|---|
| Consumer loans | Consumer loan Admnistartion fee | 1.5% of the Approved Loan Minimum TZS 10,000.00 |
| | Loan Application fee | TZS 10,000.00 |
| Wastaafu Loans | Loan Administration fee | 1.5% Minimum TZS 10,000.00 Maximum TZS 100,000.00 |
| | MIC loan Application fee | TZS 25,000.00 |
| Other Charges On individual Micro Credit | MIC loan processing/Administration fee | 1.5% Minimum TZS 50,000.00 |
| | Loan Applicationfee for Business and Personal Loans | TZS 50,000.00 |
| Interest Rates and Charges On Business Loan | Loan Administration fee- Business and Personal loans | 1.5% of the Approved Amount |

| LETTER OF CREDIT ISSUED BY OTHER BANKS (EXPORT LCS) | CHARGES |
|---|---|
| Advising Fee or commission | USD 200 or foreign eqv |
| Bank client for LC available with us | USD 150 or foreign eqv |
| Client for LC available with other Bnaks | N/A |
| Non Bank Customer | USD 250 or foreign eqv |
| Confirmation Fee(per quarter)USD eqv | 1% per quarter and part thereof,Min USD 250 or foreign eqv |
| Amendment advising Fee | USD 120 or foreign eqv |
| Cancellation Fee | USD 60 or foreign eqv |
| Transfer Fee (per quarter) | 0.75% per quarter, Min USD 250 or foreign eqv |
| Courier services | Actual costs plus USD 10 or foreign eqv |
| Swift charges | USD 60 or foreign eqv |
| Document Handling commission | N/A |
| Discrepancy Fee per document | N/A |

| LETTER OF CREDIT ISSUED BY OTHER BANKS (EXPORT LCS) | CHARGES |
|---|---|
| Commission on LC discounting/Negotiation | 0.75% Min USD 200 Max 600 or foreign eqv |
| Negotiation Bills under an Export Letter of Credit (Discounting Bills) | N/A |
| Extension - Commission for unconfirmed LC | 0.5% per quarter and part thereof, Min of USD 200 or foreign eqv |
| Extension - Commission for confirmed LC | 1% per quarter and part thereof Min. of USD 100 or foreign eqv |

| COLLECTION (DOCUMENTARY CREDIT) | CHARGES |
|---|---|
| Documents processing | 1% Min USD 15 Max 200 |
| Courier services | Actual cost plus USD 10 |
| **Outward Documentary bills for collection (OFBC)** | |
| Document handling commission | 0.5% Min USD 150 Max USD 350 or foreign eqv |
| Courier services | Actual cost plus USD 10 or foreign eqv |
| Chaser/Tracer | USD 60 or foreign eqv. |
| **Inward Documentary bills for collection** | |
| Bill discounted handling commission | 0.5% Min USD 150 Max USD 600 or foreign eqv |
| Document returned unpaid or unaccepted | 0 |
| For each amendment of previous instructions | 0 |
| Every presentation or reminder protest fee | 0 |
| Delivery of documents for non - customers | USD 250 or foreign eqv |
| Swift charges | USD 60 or foreign eqv. |
| Payment commission for documents value greater than USD 50,000 | 0 |
| Payment commission for documents value less than USD 50,000 | 0 |
| Avalisation commission per quarter or part thereof | 1.20% |
| Risk margin on acceptance (per quarter) | 1.20% |

### GUARANTEE

| COLLECTION (DOCUMENTARY CREDIT) | CHARGES |
|---|---|
| Issuance or confirmation of foreign Currency guarantee Commission(per quarter) | 1.0% per quarter or part thereof Min TZS 250,000 or USD 110, foreign eqv |
| Issuance of guarantee commission (per quarter) for Bid bond | 1.0% Bid bond Issuance part thereof Min TZS 150,000 of USD 64 foreign eqv |
| Issuance of guarantee commission (per quarter) for Perfomance,Advance Payment and any other bank guarantees | 1.0% per quarter or part thereof Min TZS 350,000 or USD 150, foreign eqv |
| Amendment fee per quarter on the tenor extended or amount increased | 1.0% per quarter or part thereof Min TZS 250,000 or USD 110, foreign eqv |
| Text amendment fee | TZS 150,000 or USD 64 or foreign eqv. |
| Other amendments | USD 60 or foreign eqv |
| Guarantee advisisng fee (from other Banks) | USD 200 or foreign eqv |
| Courier services (Direct delivery to Beneficiary) | 0 |
| Open ended guarantees(charged per annum) | 3%p.a |
| Cancellation | TZS 150,000 or USD 64 or foreign eqv. |

Tanzania Commercial Bank — Growing stronger together




Do more with our TCB Bank Popote Visa Debit Card

Accepted at all Visa outlets Point of Sales (POS) and Online platforms worldwide

Apply for your Popote Visa card at your nearest TCB Bank branch/online

Huduma kwa Wateja: +255 22 787 669977, +255 788767683, +255 658 767683, Namba bila Malipo: 0800110160 Website: www.tcbbank.co.tz

Makao Makuu, PSSSF, Millenium Towers II, Barabara ya Bagamoyo, S.L.P. 9300, Dar es Salaam, Tanzania. Simu +255 22 2162940, Faksi +255 22 2114814

Huduma kwa Wateja: +255 22 787 669977, +255 788767683, +255 658 767683
Namba bila Malipo: 0800110160

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tunataka uwajibikaji MSD maelekezo yametosha

**JANA** Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, aliiagiza Bodi ya Wakurugenzi ya Bohari ya Dawa (MSD) kufumuliwa na kusukwa upya ndani ya miezi sita, ikiwamo kuondoa watumishi waliokaa zaidi ya miaka 20.

Alisema kumekuwapo na tuhuma kubwa za rushwa MSD na licha ya kuondoa wakuu wa idara bado kunahitajika mabadiliko makubwa ili kuiunda upya.

Sio mara ya kwanza kwa serikali kutoa maelekezo ya kufumua MSD, imekuwa ikijirudia.

Mei 9, mwaka huu, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alifanya ziara MSD na kuagiza watuhumiwa wote wa ubadhirifu kama ulivyoainishwa na CAG wachukuliwe hatua, huku akiahidi kuwa TAKUKURU inafanyia kazi hoja zote zilizotolewa kuhusu bohari hiyo.

Aprili 14, mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan, alimteua Ofisa Mwandamizi wa Kampuni ya PricewaterhouseCoopers (PWC), Slaa kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya MSD.

Pia alimteua Kiongozi Mkuu wa mradi wa USAID Global Health Supply Chain Technical Assistance, Ali Tukai, kuwa Mtendaji Mkuu wa MSD.

Alitaka uwajibikaji kwa MSD ili kuwahudumia wananchi hasa kwa kupata dawa na vifaatiba muhimu kwa kuwa serikali inaelekeza fedha nyingi eneo hilo.

Mabadiliko yaliyofanywa na Rais Samia, yalifanyika siku chache baada ya CAG, kubaini bohari hiyo ilishikilia zaidi ya Sh. bilioni 14 za hospitali kwa mwaka mzima bila kupeleka dawa na vifaa tiba.

Pia alibaini MSD ilifanya ununuzi wa vifaa tiba vyenye thamani ya zaidi ya Shilingi bilioni tisa bila mkataba halali, pia ilifanya malipo ya Sh. bilioni 3.52 kwa wazabuni sita bila kufuata taratibu na kuitaarifu Bodi ya Zabuni ya MSD.

Aidha, walifanya zabuni 23 zenye thamani ya Sh. bilioni 8.55 nje ya mfumo wa ununuzi wa umma kwa mtandao (TANePS) unaosimamiwa na Mamlaka ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma (PPRA), kinyume na matakwa ya sheria.

Walifanya malipo ya awali kiasi cha Sh. bilioni 14.89 kwa wazabuni watano bila mkataba wowote wa makubaliano mengine ambayo yalibainisha msingi wa malipo ya awali.

Aidha, waliendesha mchakato wa ununuzi na kutoa mkataba wa kusambaza 'Liquid Syrup' wenye thamani ya Sh. milioni 989 bila kushirikisha Bodi ya Zabuni ya MSD.

Pia walitumia Sh. milioni 215 kugharamia posho ya watumishi watatu waliokwenda China kwenye majadiliano ya kuleta mashine za Dialysis kwa siku 61.

Waziri Mkuu, Majaliwa alivyotembelea alisema walibaini kuna udhaifu wa usambazaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi licha ya kwamba wamelipwa.

Katika idara ya ununuzi walibaini kuwapo watumishi ambao sio wataalamu na kuagiza wote 16 kuondolewa na kuwekwa watumishi wenye taaluma hiyo.

Kwa maelekezo hayo, inadhihirisha kuwa kuna tatizo kubwa ambalo hata serikali inaliona ni wakati wa kufanya uamuzi ambao utakwenda kuondoa ufisadi unaodaiwa kuwapo.

Tayari CAG amethibitisha kuwapo kwa upigaji mkubwa, lakini hatua ambazo zimeendelea kuchukuliwa ikiwamo kubadilisha uongozi wa juu wa bohari hiyo, bado hazijasaidia na sasa waziri anaeleza uwapo wa upigaji uliokithiri.

Tunaamini maelekezo ya Waziri Mkuu ni ya juu zaidi kuliko ya waziri wa sekta husika, kuja na maelekezo mengine kabla ya kueleza yale ya awali hayajachukuliwa hatua sio jambo zuri, hivyo ni muhimu serikali ikachukua hatua za utatuzi wa kudumu.

Kama tatizo limeonekana basi lishughulikiwe kwa kutumia mihimili muhimu ya serikali ambayo inaona kila mahali ili kuondoa majadiliano ya mara kwa mara kuhusu MSD huku wananchi wakiumia kwa kukosa vifaa tiba na dawa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com





Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Rais kuonya bodaboda, wenye masikio wasikie

**BODABODA** ni ujasiriamali unaowaondoa vijana wengi wanaoishi mijini na miji midogo kwenye uzururaji, maisha vijiweni na aina zote za uhalifu.

Kazi hiyo imewaweka barabarani kwa ajili ya kutoa huduma ya usafiri kwa abiria ikiwa ni ajira inayowawezesha kumudu maisha yao.

Pamoja na fursa hiyo, kumekuwapo na kasoro zinazowakabili madereva hao wa bodaboda, ikiwamo tuhuma za kusababisha ajali za barabarani zinazopoteza maisha yao na ya abiria au ulemavu wa kudumu.

Wanatuhumiwa kutumika kwenye ujambazi wakiendesha pikipiki zilizoibwa na madereva wake kuuliwa, wapo wanaodaiwa kukwapua mali za watu hasa pochi na mifuko ya wanawake vilevile kunyanyasa wanafunzi kingono.

Ni mambo yanayochangia ajira hiyo kuwa chungu iwapo hawatabadilika. Mienendo yao imemshtua Rais Samia Suluhu Hassan, na kutoa onya dhidi ya kutumika kwenye ujambazi pamoja na uhalifu ili kulinda heshima yao.

Rais Samia anabainisha kuwa baadhi ya madereva wa bodaboda wamekuwa wakikwapua mizigo ya watu pamoja na vipochi hasa vya wanawake na kupoteza uaminifu mbele ya jamii.

"Ninyi ni maofisa usafirishaji wa kitaifa lakini baadhi yenu wanawaharibia sifa hiyo kwa kutumika kukwapua na kupoteza mizigo ya watu pia, kutumika kwa ujambazi. Niwaombe, jilindeni msipoteze sifa zenu nyie ni watu muhimu sana katika taifa letu,"anasema Rais Samia.

Rais amekerwa na tatizo hilo, hivyo ingefaa kila bodaboda kuachana na mtindo huo ambao unaweza kutishia ajira na maisha.

Ingawa Rais amewaomba waache mtindo huo, ni vyema pia wakatambua kuwa hilo si ombi ni amri, hivyo wangetii na kuendesha shughuli zao kama kawaiada bila kusubiri kushurutishwa.

Anayosema Rais ni kweli, kwa vile unapotajwa usafiri kwa wanyonge bodaboda zinahusika, kusafirisha watu kwa gharama nafuu, hivyo ingependeza kama wangeheshimu ajira hiyo.

Wakumbuke kuwa awali walikuwa wakitozwa faini ya Sh. 30,000 wanapofanya makosa ya barabarani, lakini wakalia kilio chao, wabunge wakawatetea hadi kiwango hicho kikashushwa.

Hatua hiyo ya kushushiwa faini, inaonyesha ni jinsi gani ajira yao inavyoheshimiwa, hivyo na wao waiheshimu kwa kuachana na uhalifu.

Binafsi nilishwahi kukumbana na dereva mporaji saa 11 alfajiri nikiwa katika kituo cha daladala nikisubiri usafiri, akaja huku akionyesha kama mtu mwema na kuniambia nitoe nauli kidogo anisafirishe ninakokwenda.

Lakini kabla ya kumjibu akakwapua mfuko wangu na kujikuta akiambulia mkanda na kuondoka, lakini baadaye akageuza bodaboda yake akaja na kunirushia mkanda huo na kuondoka zake.

Huo ndiyo mtindo wa baadhi ya madereva wa bodaboda, ingawa baadhi yao hudai kuwa wanaofanya hivyo ni 'deiwaka' si wale wanaoendesha pikipiki na kwamba hupewa ili kujitafutia chochote lakini badala yake wanapora watu.

Kama kweli wanaofanya hivyo ni 'deiwaka', basi walioajiriwa kufanya kazi hiyo wasikubali kuharibiwa sifa kwa huruma za kutaka kuwasaidia marafiki zao wajipaatie riziki kupitia pikipiki hizo na kumbe wanazitumia kuibia watu.

Udereva wa bodaboda ni ajira, ingekuwa ni njia sahihi iwapo madereva wake wataheshimu ajira hiyo kwa kuepuka kujiingiza katika matendo ya uhalifu yanayohatarisha ajira hiyo.

Onyo la Rais Samia kwao litoshe kuwafanya wabadilike, kwani hayo ndiyo matarajio ya kiongozi huyo wa taifa kwa wananchi wake hasa kwa kundi la waendesha bodaboda.

Vilevile, onyo hilo lingewakumbusha pia kuheshimu sheria ya usalama barabarani,kwani wamekuwa wakitajwa kuwa vinara wa kuvunja sheria hiyo na kusababisha ajali.

Kwa mfano, wanapofika kwenye makutano ya barabara, kwenye taa hata kabla hazijawaruhusu kupita, hulazimisha kuivuka upande wa pili hali ambayo imekuwa ikichangia ajali za barabarani.

Wasikie onyo vingine wanajiweka kwenye hatari ya kuwa na migogoro na sheria.

TANGAZO

TANESCO KATIKA MWELEKEO CHANYA

# TANESCO katika mwelekeo chanya wa kukidhi mahitaji ya umeme nchini ifikapo mwaka 2030

**Na Valentine Oforo, Dodoma**

UZALISHAJI, usafirishaji na usambazaji wa nishati ya umeme wa uhakika katika maeneo yote ya nchi ni miongoni mwa sekta muhimu katika kuchochea kasi ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii, na hivyo kuiwezesha Serikali kufikia maono ya uchumi iliyojiwekea ifikapo mwaka 2025.

Kwa mtazamo rahisi, maono ya maendeleo ya kiuchumi ambayo Tanzania inaazimia kuyafikia ifikapo mwaka 2025, kwa kiasi kikubwa yanategemea utendaji na ubunifu wa uongozi wa Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania (TANESCO) katika kuwaongoza wafanyakazi wake kutekeleza majukumu yao kwa uweledi, uzalendo na juhudi ya hali ya juu.

Hata hivyo, tangu kuanzishwa kwake mwaka 1964, TANESCO imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuweka rekodi nzuri ya utekelezaji wa miradi muhimu ili kuhakikisha watanzania wanaoishi vijijini na mijini wanafikiwa na huduma ya nishati ya umeme, hatua muhimu ambayo hadi sasa imechochea kasi ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii, hususan katika uwekezaji wa viwanda vidogo, vya kati na vikubwa.

Wakati takwimu zinaonyesha kwamba mahitaji ya umeme nchini Tanzania yanatarajiwa kupanda kutoka Gigawatt (GWh) 10,176 hadi 28,663 ifikapo mwaka 2030, ikiwa ni asilimia 13.82 ya kiwango cha ukuaji wa kila mwaka (CAGR), TANESCO kwa upande wake tayari imeanza kuchukua hatua mbalimbali za kukidhi mahitaji ya umeme yanayotarajiwa kuongezeka, ikiwa ni pamoja na mkakati unaoendelea unaolenga kuongeza uzalishaji wa megawati 9000 za umeme ifikapo mwaka 2030.

Hata hivyo, mahitaji ya umeme nchini Tanzania yanakadiriwa kukua kwa wastani wa kati ya asilimia 10 na 15 kwa mwaka, na kwa kuzingatia kwamba kwa sasa ni asilimia 24 tu ya watanzania ndiyo wanaopata umeme, TANECO imejipanga vyema kuongeza uwezo wa uzalishaji wa umeme nchini, kutoka megawati 1,695 zinazozalishwa kwa sasa hadi kufikia megawati 5,000 ifikapo 2025.

Pamoja na jitihafa hizo, ili kufikia azma hiyo, serikali imeanza kufanya mageuzi katika Sekta ya Ugavi wa Umeme (ESI) hasa kwa kuvutia mitaji binafsi katika sekta hiyo muhimu.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mkuu wa TANESCO, (MD) Maharage Chande, Shirika hilo la umma kwa sasa linafanya kazi usiku na mchana ili kuvumbua na kutumia mifumo ya kisasa zaidi ya kidigiti kwa lengo la kuboresha utoaji wa huduma za nishati nchini na kwa viwango vya kimataifa.



*Jengo la kuendeshea mitambo katika ujenzi wa mradi wa kufua umeme wa Julius Nyerere unaojengwa katika mto Rufiji, mkoani Pwani. . Picha: Valentine Oforo*

"Ili kuongeza kasi ya utoaji huduma kwa wateja, tumefanikiwa kuanzisha mfumo wa kisasa wa kidigiti, ujulikanao kama 'NIKONEKT', ambao ni jukwaa muhimu la mtandaoni kwa ajili ya kuwasaidia wateja kutuma maombi, na kuunganishiwa huduma za umeme wakiwa majumbani mwao bila haja ya kufika kwenye Ofisi zetu mbalimbali ndani ya nchi," Chende alileza.

Pamoja na hayo, Chande aliongeza kuwa uanzishwaji wa kituo maalum cha kupokea miitikio ya simu chenye uwezo wa kurekodi mazungumzo kati ya TANESCO na wateja wake ni hatua nyingine muhimu waliyofikia katika azma ya kuboresha huduma kwa wananchi, na kubainisha kuwa huduma hiyo tayari inatumiwa na wateja katika mikoa 13 ya kanda ya mashariki na kaskazini pamoja na mikoa ya nyanda za juu kusini.

"Malengo tuliyojiwekea ni kuhakikisha kwamba mpaka ifikapo mwishoni mwa mwaka huu huduma hii ya miitikio ya simu iwe imewafikia wateja wetu katika mikoa yote hapa nchini," Mkurugenzi aliongeza.

Hata hivyo, ili kuimarisha miundombinu ya kusafirisha na kusambaza umeme, Maharage amesema kwa sasa TANESCO imeamua kujikita zaidi katika matumizi ya nguzo za umeme za zege, hasa katika utekelezaji wa miradi ya njia za umeme zenye msongo wa kilovolti 1, 33 na 66, na kuongeza kuwa nguzo za mbao zitatumika katika mitandao ya umeme ya nguvu (voltage) ndogo.

"Matumizi ya nguzo za zege za saruji yatatusaidia kuondokana na changamoto za kusafirisha umeme katika maeneo yenye maji na yenye wanyama," alisisitiza.

Akieleza juu ya jitihada katika kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabia nchi ambazo mara nyingi zimekuwa zikikwamisha jitihada za usambazaji wa umeme kwa urahisi, Chande alieleza kuwa, TANESCO kupitia kampeni maalumu ya 'TUNAJIPANGA' inatekeleza miradi kadhaa ya kusaidia kupanua uwezo wa kuzalisha umeme miongoni mwa vituo vyake vingi hapa nchini.

Aidha, katika mwendelezo wa utendaji kazi mahiri unaotumia kaulimbiu ya 'Tunayaangazia Maisha Yako', Chande amesema TANESCO kwa sasa inaendelea na kazi ya ujenzi na uboreshaji wa vituo vikubwa na vya kati vya kuzalisha na kupoozea umeme katika maeneo mbalimbali, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa vituo katika mikoa ya Kigoma, Rukwa na Katavi mikoa ambayo bado haijaunganishwa katika mfumo wa gridi ya taifa (National Grid).

"Mradi wa ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Julius Nyerere (JNHPP) katika Mto Rufiji ni mojawapo ya mradi mkubwa unaoendelea ambao tunautekeza kwa malengo mapana ya kuongeza huduma za uzalishaji na usambazaji wa umeme nchini Tanzania. Mradi kwa sasa umefikia asilimia 62.95 ya utekelezaji wake na utakapo kamilika unatarajia kuzalisha kiasi cha megawati 2115," aliongeza.

Chande, amemshukuru Raisi Samia Suluhu Hassan kwa jitihada kubwa katika kuliwezesha shirika hilo kufanya kazi kwa ufanisi, hususan kwa kulitengea fedha za kutosha za kusaidia utekelekzaji wa miradi muhimu.

Kutokana na kuthibitisha ubora na dhamira njema katika utoaji wake wa huduma za umeme, serikali katika mwaka wa fedha 2022/23 iliamua kutenga jumla ya shilingi bilioni 500 ili kuongeza uwezo wa TANESO katika kuboresha utoaji wa huduma za umeme nchini, lengo likiwa kukidhi uwezo wa kufikisha nishati hiyo katika maeneo yote ya nchi.

January Makamba, wazairi wa Nishati, mbali na kuipongeza TANESCO kwa kazi nzuri, amesema serikali ya awamu ya sita imejipanga kuhakikisha shirika hilo linaboresha ufanisi kwa kiasi cha kuwa kati ya mashirika bora ya ugavi wa huduma za umeme barani Afrika.

Kupitia fedha hizo, shilingi bilioni 500, Waziri Makamba ameeleza matumaini kwamba TANECO itakuwa katika nafasi nzuri ya kuboresha huduma zake, hasa katika kuwafikia watanzania wengi zaidi.

"Pamoja na jitihada nyingine, kwa mwaka huu wa fedha TANESCO inatarajia kutekeleza mradi wa uimarishaji wa Gridi ya Taifa' pamoja na mradi mwingine unaolenga kuunganisha mikoa ya Katavi, Kigoma na Rukwa kwenye Gridi ya Taifa," Makamba amesema.

Kwa mujibu wa waziri Makamba, miradi mingine itakayotekelezwa kwa mwaka 2022/23 ni pamoja na mradi wa kuboresha mfumo wa usambazaji umeme katika Jiji la Dodoma, mradi wa njia ya kusafirisha umeme Msongo wa KV 132 kutoka Tabora hadi Urambo na kutoka Urambo Tabora hadi Kidahwe mkoani Kigoma.

"Miradi mingine inayoendelea ambayo katika siku za usoni inatarajiwa kutoa mchango mkubwa katika kuongeza upatikanaji wa umeme ni pamoja na mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kV 400 kutoka Singida – Arusha – Namanga, pamoja na Mbeya- Tunduma" Waziri aliongeza.

Kwa upande wake, Msemaji wa TANESCO, Martin Mwambene amesema hadi sasa shirika limefikia hatua kadhaa, hasa katika upande wa kuboresh uwezo wake wa kuzalisha, kusafirisha na kusambaza umeme, pamoja na huduma kwa wateja.


Alifahamisha kuwa, huduma za kidigiti za NIKONEKT zilizobuniwa na shirika hilo kwa kiasi kikubwa zimewezesha kampuni kufikia malengo makubwa katika kuwahudumia wateja wake, na kuongeza kuwa wanaendelea na mchakato wa kubuni na kutambulisha mifumo mingine rafiki ya kidigiti ya kuborsha huduma zote.

Maonesho ya biashara ya kimataifa ya Dar es Salaam (DIFT) ya mwaka huu, yaliyofanyika kuanzia Juni 28 hadi 13 Julai 2022 Jijini Dar es Salaam yalishuhudia TENESCO ikiibuka miongoni mwa makampuni yaliyofanya vizuri na hivyo kutunukiwa tuzo maalum.

TANESCO ni shirika linalohusika na ugawaji wa umeme nchini Tanzania. Shirika hili lilianzishwa mwaka 1964. Shirika la TANESCO linamilikiwa na serikali ya Tanzania. Wizara inayosimamia shughuli za TANESCO ni Wizara ya Nishati



*Makamu wa Rais, Dk.Philip Mpango (wa pili kulia) akizungumza na watendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na wa wizara ya Nishati wakati wa ziara yake ya kutembelea mradi wa kufua umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) unaojengwa katika mto Rufiji, mkoani Pwani. Picha: Valentine Oforo*



*Wafanyakazi wa kituo maalum cha miitikio ya simu cha TANESCO wakiwa katika majukumu yao ya kila siku ya kupokea simu mbalimbali kutoka kwa wateja wanaotaka kupata taarifa kuhusu huduma za shirika hilo. Picha: Valentine Oforo*

216960401

# Bei ya maharagwe yazidi kupaa Iringa

**Martha Sambo,** IRINGA

WAKATI wakulima wakiwa kwenye msimu wa mavuno, bei ya nafaka hasa maharagwe katika soko kuu la Manispaa ya Iringa inazidi kupaa kwa kasi.

Baadhi ya wafanyabiashara waliozungumza na Nipashe jana, walisema miaka mingine kama sasa bei imekuwa chini kwa kuwa ni msimu wa mavuno, lakini hali imezidi kuwa tofauti.

Wiki iliyopita maharagwe yaliuzwa kwa Sh. 1,800 kwa kilo moja lakini kwa sasa yanauzwa Sh. 2,500.

Mmoja wa wafanyabiashara, Deogratius Kipingi, alisema licha ya zao hilo kuuzwa kwa bei nafuu awali lakini kwa sasa bei yake haishikiki.

"Bei ya kununua maharagwe ni Sh. 2,000 hadi 2,100 kutoka Sh. 1,600 ya awali na debe likiwa ni Sh . 45,000 tofauti na ilivyokuwa awali," alibainisha Kipingi.

Alisema licha ya kupaa kwa bei ya maharagwe sokoni hapo pia uhaba wa maharagwe kutoka kwa wakulima inaongeza ugumu wa biashara hiyo na kuitaka serikali kutafuta mwarobaini ili kuendeleza kilimo, na biashara hasa kwenye kwa maharagwe na nafaka zingine.

Pia alisema kufunguliwa kwa mipaka ya usafirishaji wa maharagwe kwenda mikoa mingine, ni chanzo cha zao hilo kupungua sokoni, huku wakulima nao wakilia na kupaa kwa bei ya pembejeo na kuwaacha wengi wao wakishia kulima holela na kuambulia hasara.

Mkulima Laurent Inno, alisema ikiwa serikali itapunguza bei za pembejeo za kilimo itasaidia kupunguza makali kwenye upatikanaji wa zao la maharagwe sokoni na kutoa uwanja mpana kwa vijana kujizatiti katika kilimo na biashara hiyo.

"Soko la maharagwe lipo lakini, upatikanaji wa bidhaa umekuwa changamoto sana na bei ipo juu mno. Naiomba serikali itupunguzie kadhia hii ili vijana tuendelee kujiajiri na kuepuka kujiingiza katika vitendo vya kihalifu katika jamii,"alisema Laurent.

Ofisa Biashara Manispaa ya Iringa, Neema Thomas, ambaye pia ni msimamizi wa masoko katika halmashauri hiyo, alisema mabadiliko ya tabianchi yamechagiza kupungua kwa uingizwaji wa nafaka sokoni kutokana na kupungua kwa uzalishaji shambani. Aliongeza kuwa ipo haja ya wakulima kuendelea kufuata ushauri unaotolewa na maofisa ugani ili kuendana na mabadiliko ya hali ya hewa na kuondokana na kupata hasara.

Pia alisisitiza wakulima kufanya kilimo cha umwagiliaji ili kukabiliana na changamoto ya mabadiliko ya tabianchi na kujipatia mazao kwa wingi.



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makala (wa nne kushoto), akisalimiana na walimu baada ya kuzindua rasmi huduma ya Mwalimu Spesho ya Bodaboda ya Benki ya NMB, jijini Dar es Salaam jana. Wanaoshuhudia ni Ofisa Mkuu wa Biashara na Wateja Binafsi wa benki hiyo, Filbert Mponzi (wa tatu kushoto), Meneja wa Kanda ya Dar es Salaam, Donatus Richard na Mkuu wa Idara ya Wateja Binafsi Aikansia Muro. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# SBL yafungua ufadhili wanafunzi familia duni

**Na Frank Monyo**

KAMPUNI ya Bia ya Serengeti (SBL), imefungua dirisha la ufadhili wa masomo ya kilimo kwa wanafunzi wazawa wanaofanya vizuri katika masomo yao wanaotoka familia duni.

Hatua hiyo ni mwendelezo wa kuunga mkono jitihada za serikali kuendeleza sekta mama ya kilimo nchini, na kwamba hadi sasa wamefadhili wanafunzi 200 tangu mwaka 2019.

Akiongea na gazeti hili jana mkoani Dar es Salaam, Mkurugenzi wa Uhusiano kwa Umma wa SBL, John Wanyancha, alisema ufadhili huo ni kupitia programu ya Kilimo Viwanda na kwamba wanakaribia kufungua dirisha la maombi kwa wanafunzi wanaofanya vizuri darasani.

"Dirisha la maombi linatarajiwa kufunguliwa hivi karibuni na kutaka nafasi kwa vijana wote wa Tanzania kutumia fursa hii katika kuleta mapinduzi ya kilimo, na kuipa uhai azma ya kutengeneza uwanja wa kilimo na biashara.," alisema.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, lengo ni kuleta mapinduzi ya kilimo na kwamba ufadhili huo utaongeza nguvu katika muhimili wa utafiti na maendeleo ya kilimo kwa kuleta wataalamu wa kilimo wanaoendana na mazingira halisi ya uzalishaji na ubunifu wa mbinu za kilimo.

"SBL imeshirikiana na vyuo vinne vya kilimo nchini ambavyo ni pamoja na Chuo cha Kilimo cha Mt. Maria Goretti mkoani Iringa, Chuo cha Kilimo na Mafunzo ya Kilimo na Ufugaji Kilacha Kilimanjaro, na Chuo cha Kilimo Kaole Wazazi kilichopo Bagamoyo na chuo cha Igabiro, Muleba mkoani Kagera.

"Maofisa ugani wana mchango mkubwa sana katika kuongeza thamani na kuleta mabadiliko ndani ya sekta ya kilimo. Wanafunzi watakaohitimu kupitia programu ya kilimo na viwanda, wanatarajiwa kurudi mashambani na kuwapa wakulima elimu, maagizo na taratibu maalumu za kufuata ili kuongoza uzalishaji," alisema.

"Tunaamini katika programu hii kwenda mbali sana katika kuongeza nguvu ndani ya wigo wa wataalamu wa kilimo nchini, jambo muhimu katika kuwasaidia wakulima kuongeza uzalishaji na kipato chao," aliongeza.

## Viongozi watakiwa kusimamia Sheria za Misitu

**Na Christina Haule,** MOROGORO

VIONGOZI wa serikali kuanzia ngazi za vijiji hadi wilaya mkoani hapa wametakiwa kuhamasisha na kusimamia jamii kufuata sheria za misitu zilizoko wanapoandaa mashamba ili kuepuka ukataji miti ovyo unaosababisha upotevu wa misitu.

Mhifadhi Mwandamizi wa Wakala wa Huduma za Misitu (TFS), Manispaa na Wilaya ya Morogoro, Faustine Msokwa, alisema jana kuwa jamii haiangalii mambo ya maendeleo ya baadaye kwao na taifa kwa ujumla bali hukata miti kwa madai ya kusafisha mashamba kwa manufaa ya fedha za muda mfupi.

Alisema suala la ukataji miti ovyo na uchomaji mkaa linasababishwa na viongozi wa vijiji ambao ndiyo wana umiliki wa ardhi za vijiji wanaozitoa kwa wakazi wao bila kuweka msisitizo ikiwamo wa matumizi ya ardhi hiyo kuwa endelevu baada ya misitu kukatwa.

Msokwa alisema Usimamizi Shirikishi wa Mazao ya Misitu (USMJ), unataka ushiriki wa wadau wote wa misitu ambao ni pamoja na wakulima na wafugaji ambao wanavamia maeneo na kudai wanasafisha kwa kilimo au kukaa na mifugo huku wakikata miti ambayo inatakiwa kuhifadhiwa kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo.

"Huwa tunawakamata waharibifu wa misitu hata 40-50 shambani wakidai wanaandaa mashamba kwa kuwa wana kibali cha kijiji, lakini ukifuatilia miti wanayokata wanachoma mkaa na utakuta wenye kibali cha kusafisha shamba ni wawili au watatu pekee, jambo ambalo ni hatari katika uhifadhi wa misitu," alisema Msokwa.

Alisema suala la ukataji miti ovyo na uchomaji wa mkaa bila kufuata utaratibu linaifanya manispaa na wilaya kushindwa kukadiria kiwango cha mkaa kinachofaa kutumika kwa jamii husika.

Hata hivyo, alisema upo mkanganyiko unaorudisha nyuma suala la USMJ ikiwamo sera mtambuka za wizara ya misitu zinazohamasisha uhifadhi wa misitu wakati kilimo kinahamasisha wakulima kupanua mashamba kwa ajili ya kilimo endelevu.

Aidha, Msokwa aliihamasisha jamii kujitokeza kupata elimu ya ufugaji nyuki na kupata mizinga bure kutokana na ufugaji wa nyuki kuwa na faida kubwa, mfugaji anaweza kuvuna asali kila baada ya miezi 3-6 kwa mwaka na kupata masoko ya ndani na nje ya nchi.

Msokwa alisema hamasa ya ufugaji nyuki katika Wilaya ya Morogoro ni ndogo kutokana na ukosefu wa elimu na TFS ipo tayari kumsaidia mtu mmoja mmoja au kikundi kielimu ,na mizinga bure iwapo atajitokeza ili aweze kufuga nyuki na kuhifadhi mazingira.

## Benki yachochea uchumi wa kusini

**Na Mwandishi Wetu,** MTWARA

BENKI ya Exim Tanzania, imeelezea azma yake ya kukuza na kuchochea ukuaji wa uchumi katika mikoa ya Lindi na Mtwara, kwa kuunga mkono jitihada za kukuza sekta ya kilimo, biashara na elimu katika mikoa hiyo.

Katika kuthibitisha azma yake hiyo, viongozi waandamizi wa benki hiyo wakiwamo Mkuu wa Huduma ya Rejareja wa benki hiyo, Andrew Lyimo, na Mkuu wa Masoko na Mawasiliano, Stanley Kafu, mwishoni mwa wiki walitoa msaada wa madawati 200 kwa baadhi ya shule za mikoa hiyo na chakula cha jioni na wateja.

Hatua hiyo ilitoa fursa kwa benki hiyo kuelezea huduma zake mpya, fursa za biashara pamoja na mkakati wake katika kukuza sekta za elimu pamoja na kilimo husasani kupitia zao la korosho.

Akizungumza kuhusu matukio hayo, Lyimo alisema yametoa fursa kwao kukutana na wateja wao, viongozi waandamizi wa serikali na wadau wengine muhimu, kupata mrejesho wa mahitaji ya wateja.

"Mtwara na Lindi ni miongoni mwa mikoa muhimu sana kwetu kibiashara na hiyo ndiyo sababu ilikuwa miongoni mwa mikoa ya awali kabisa kufungua matawi yetu,"alisema.

"Katika kipindi chote cha uwapo wetu katika mikoa hii, tumekuwa na mchango mkubwa kwa wakazi wa mikoa hii kwa kutoa huduma zinazowalenga haswa ikiwamo mikopo ya kilimo, biashara, mikopo ya watumishi na sasa tumekuja na huduma mahususi kwa ajili ya wajasiriamali," aliongeza.

Alisema hali ya uchumi katika mikoa hiyo kupitia uboreshwaji wa Bandari ya Mtwara inazidi kutoa fursa kubwa kwa benki hiyo kuhudumia wateja zaidi wakiwamo wafanyabiashara wakubwa na wa kati kutoka ndani na nje ya nchi ambao wanatumia bandari hiyo.

"Uwapo wa Benki ya Exim katika visiwa vya Comoro unatoa fursa kwa wafanyabiashara wa pande hizi mbili kufanya biashara kwa urahisi zaidi kwa kuwa Exim tunawahakikishia huduma za uhakika za kifedha ikiwamo mikopo," alisema.

Kwa upande wake, Kafu alisema mchango wa benki hiyo katika mikoa hiyo haujaishia katika utoaji wa huduma za kifedha bali pia imekuwa mdau muhimu wa maendeleo ya kupitia mpango wake wa uwajibikaji kwa jamii ujulikanao kama Exim Cares.

"Serikali kupitia viongozi mbalimbali wanafanya jitihada kubwa kuboresha sekta mbalimbali ikiwamo elimu, afya na kilimo hivyo ni jukumu letu sisi kama taasisi za kifedha kuunga mkono jitihada hizo za serikali,"alisema.

"Kupitia mkakati huu uliozinduliwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa mwishoni mwa mwaka jana tumeweza kutoa msaada wa madawati katika mikoa mbalimbali hadi sasa ikiwamo mikoa ya Dodoma, Mbeya, Mwanza, Shinyanga, Tabora, Lindi na Mtwara na bado tunaendelea mikoa mingine zaidi," alisisitiza.

# CRDB yazindua tawi Wete, wananchi wapewa mikopo

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, amezindua tawi jipya la Benki ya CRDB na kukabidhi pikipiki na boti za uvuvi na kilimo ili kuwashirikisha wananchi wengi kuujenga uchumi wa visiwa hivyo.

Juzi Dk. Mwinyi alikabidhi jumla ya pikipiki 272 na boti 94 zitakazosaidia kuimarisha shughuli za vijana na wanawake ambazo ni mkopo uliotolewa na Benki ya CRDB.

"Tuliahidi na sasa tunatekeleza. Mtakumbuka siku chache baada ya kuapishwa kuingia madarakani, niliziomba taasisi za fedha kushirikiana na serikali kufanikisha utekelezaji wa ahadi nilizozitoa kipindi cha kampeni za uchaguzi mkuu.

"Benki ya CRDB imekuwa mstari wa mbele katika hili na leo (juzi) tumeanza na vijana pamoja na wavuvi na wakulima wa mwani," alisema.

Rais Dk. Mwinyi alizindua mikopo hiyo kwenye ufunguzi wa tawi la Benki ya CRDB lililoko katika Mtaa wa Sunda, Barabara ya Mtemani, akiwahimiza wananchi kuzitumia huduma zake kufanikisha shughuli zao za kiuchumi.

"Tawi hili linatoa huduma za benki kwa masharti ya kiislam na yale ya kawaida. Serikali kwa kushirikiana na wadau, imedhamiria kuwawezesha wananchi kiuchumi, ndiyo maana inasogeza huduma zikiwamo za kifedha jirani yenu. Kila mmoja aangalie fursa zilizoko kukuza uchumi wake," alisisitiza Rais Dk. Mwinyi.

Alipozindua kampeni zake Septemba 12, 2020 kwenye Uwanja wa Demokrasia ulioko Kibandamaiti mjini Unguja, Dk. Mwinyi aliahidi mambo kadhaa ya kuyafanyia kazi akiwa Rais, ikiwamo kuimarisha uchumi wa buluu, kilimo na kuwawezesha wananchi kwa mitaji.

Kati ya pikipiki 272 zilizokabidhiwa juzi, 222 zilitolewa kwa vijana wa Mkoa wa Pemba Kaskazini na 50 kwa Pemba Kusini huku mkoa ukipata nusu ya boti 94 zilizokuwapo ambazo 32 ni kwa ajili ya kilimo cha mwani na 15 kwa ajili ya uvuvi.

Vilevile, Rais alikabidhi hundi za mkopo kwa vikundi vitatu zenye thamani ya Sh. milioni 273.8. Mikopo hiyo ilitolewa kwa Chama cha Ushirika Shirikani (Sh. milioni 210.8), Chama cha Ushirika Umoja ni Nguvu (Sh. milioni 58.8) na Chama cha Ushirika Mategemeo kilichopokea Sh. milioni tano.

Mnamo Februari mwaka huu, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) iliingia makubaliano na Benki ya CRDB kuwakopesha wananchi bila riba ikiikabidhi benki hiyo Sh. bilioni 60 zitakazokuwa zikitolewa kila mwaka kwa kipindi cha miaka mitano mfululizo.

Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB, Abdulmajid Nsekela, alibainisha kuwa kuanzia Januari hadi Juni mwaka huu, wamekopesha Sh. bilioni 23.5 kwenye matawi matatu yaliyokuwapo na anaamini wananchi wa Wete sasa wanayo fursa ya kulitumia tawi hilo linalofanya jumla kuwa manne visiwani hapa.

"Wananchi wanaweza kupata huduma zetu pia kupitia mawakala 280 tulionao Unguja na Pemba. Mheshimiwa Rais, ulitupa changamoto ya kusogeza huduma kwa wananchi na leo (juzi) tumefika Wete," Nsekela alitamba.

Mkurugenzi huyo alisema wataendelea kushirikiana na serikali kufanikisha miradi ya maendeleo, ukiwamo utekelezaji wa programu ya Inuka na Uchumi wa Buluu inayolenga kuwawezesha wananchi kunufaika na fursa zilizoko baharini.

Nsekela alibainisha kuwa kati ya Sh. bilioni 60 zilizotolewa na serikali, Sh. bilioni 6.7 zimekopeshwa kwa vikundi 607, vikiwamo 58 vya wilayani Wete. Vikundi hivyo vyote vina wanachama 11,806, wakijumuisha 689 wa Wete waliopokea Sh. milioni 529.6.

Akizungumzia umuhimu wa sekta binafsi katika kujenga uchumi, Waziri wa Fedha na Mipango wa SMZ, Dk. Saada Mkuya, alisema taasisi za fedha zinachangia asilimia 3.4 kwenye Pato la Taifa kwa mwaka.



Mmoja wa wanawake akikusanya mawe aliyoyachonga katika machimbo ya Nyashana, kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya mawe ya Nyanda ya mita 370, eneo la Igoma, jijini Mwanza, wakati wajumbe wa Bodi ya Mfuko wa Barabara (RFB), walipokagua machimbo hayo, juzi. **PICHA: NEEMA EMANNUEL**

# Jela miaka saba kuua bila kukusudia

**Christina Haule,** MOROGORO

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Morogoro imemhukumu kifungo cha miaka saba jela Donati Phabian baada ya kupatikana na hatia ya kumuua bila kukusudia Alfred Damas kwa madai ya kumkuta akizungumza na mtalaka.

Phabian alifanya kitendo hicho baada ya kuwakuta wawili hao barabarani katika kijiji cha Lugangwa, Tarafa ya Matombo wilayani Morogoro.

Akisoma hukumu hiyo, Jaji Paulo Ngwembe alisema amezingatia kwa kina mazingira yaliyosababisha mauaji hayo na kuona kuwa ni mazingira ya kukosekana kwa utu.

Jaji alisema mshtakiwa aliamua kujichukulia sheria mkononi kwa kumuua mwanamume aliyemkuta amesimama njiani akizungumza na mwanamke ambaye yeye alikuwa mke wake huku akiwa tayari ameshampa talaka.

Licha ya mshtakiwa kufika kituo cha polisi kujielezea kuwa alifanya hivyo kwa sababu bado ana mapenzi na mkewe na asingependa awe na mtu mwingine, alisema hilo ni jambo la mapenzi ya kitoto na kwamba kama angetaka usuluhishi angeenda mbele ya wazazi wao.

Alisema kimsingi inaonyesha mshtakiwa alijipeleka polisi kwa kulinda usalama wake na si kujutia makosa yake kwamba adhabu hiyo ya miaka saba jela, itamfanya ajutie makosa yake na kuwa fundisho kwa wengine.

Hata hivyo, Jaji Ngwembe alisema hati ya kukata rufani dhidi ya adhabu hiyo iko wazi kwa mshtakiwa pale atakapotaka kufanya hivyo.

Awali, Wakili wa Utetezi, Kisawai Mandela, aliiomba mahakama kumpa mshtakiwa adhabu yenye huruma kwa sababu ni mtendaji kosa kwa mara ya kwanza na ana watoto ambao wanamtegemea.

Naye Wakili wa Serikali, Evelyne Ndunguru, aliiomba mahakama kumpa mshtakiwa adhabu itakayolingana na kosa alilolitenda ili iwe fundisho kwake na wengine wenye tabia za kujichukulia sheria mkononi.

Akisoma shtaka, karani wa mahakama hiyo, Lilian Kombe, alidai kuwa mshtakiwa alifanya kosa hilo mwaka 2021 kwa kumuua mwanamume wa mke wake aliyemwacha kwa kumchanja na kisu mwilini mbele ya ndugu wawili wa mwanamke huyo, jambo lililosababisha kifo chake papo hapo.

Wakati huo huo, Amelda Ngagiri (60) mkazi wa kijiji cha Nyandira, wilayani Mvomero amehukumiwa kifungo cha nje kwa miezi 12 na kupewa adhabu ya kusafisha eneo la kituo cha afya Nyandira baada ya kupatikana na hatia ya kuua bila kukusudia.

Jaji Ngwembe alisema ameamua kutoa hukumu hiyo kwa mshtakiwa huyo kutokana na umri wake mkubwa na afya yake kuwa si nzuri na kwamba anapaswa kusafisha kituo hicho na akishindwa atakwenda jela miaka minne.

Awali karani Lilian Kombe alidai kuwa tukio hilo lilitokea Mei 25, 2020 majira ya usiku katika kijiji cha Nyandira ambapo mshtakiwa huku akijua kufanya hivyo ni kosa, alimuua kwa kumshambulia na gongo aliyekuwa amelewa.

# SHIVYAWATA yapongeza kushirikishwa kwenye sensa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

SHIRIKISHO la Vyama vya Watu Wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA) wilayani Kahama, limeipongeza serikali kwa kuwashirikisha kwenye sensa ya watu na makazi ili kuhakikisha makundi yote maalumu yanafikiwa na kuhesabiwa.

Katibu wa SHIVYAWATA Kahama, Zawadi Masoud, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na vyombo vya habari ofisini kwake namna watashirikiana katika sensa ya watu na makazi.

Alisema wanafahamu namna ya kuzungumza na watu wasiosikia, wasiona na viziwi kwa kutumia lugha za alama ikiwa ni pamoja na kuzitambua kaya zenye watoto na watu wenye ulemavu, hivyo ushiriki wao utakuwa rahisi na makundi hayo kuhesabiwa kwa pamoja.

Masoud pia alisema familia nyingi zinawaficha ndani watoto na watu wenye ulemavu kwa sababu ya mila potofu iliyojengeka vichwani mwao kwamba wakizaa mtoto mwenye ulemavu ni laana na wanaogopa kuwatoa ndani kwa kuhofiwa kuchekwa na jamii zinazowanguka.

"Kuna baadhi ya kaya hapa Kahama baba au mama ni mtu wenye ulemavu wa kusikia na kuzungumza naye, hivyo inahitajika mtu mwenye kujua lugha za alama. Je, siku ya kuhesabiwa sensa kutakuwa na mtu wa namna hiyo ili azungumze nao? Ndiyo sababu yao kushirikishwa, alisema.

Hata hivyo, aliomba kama kuna watu wenye ulemavu waliomba nafasi za uwakala wakati wa siku ya sensa, basi wapewe kipaumbele kwa sababu wao watasaidia kuwabaini watu wenye ulemavu na kuhesabiwa au wawasiliane na viongozi ili kuwapata makarani hao ili sensa ifanyike ipasavyo bila kumruka mtu yeyote.

Naye Mjumbe wa SHIVYAWATA, Edward Charles, alisema baadhi yao hawafahamu umuhimu wa sensa kulingana na hakuna mtu wa kuwafikia na kuwapatia elimu na watu wanaoweza kuwafikia na kuzungumza nao ni wao wenyewe au mtaalamu wa lugha ya alama.

Charles aliwaomba maofisa maendeleo ya jamii ngazi za halmashauri na kata, mitaa, vitongoji na vijiji wanapokwenda kutoa elimu hiyo ndani ya jamii, wahakikishe wanawashirikisha viongozi wa vyama vya watu wenye ulemavu ili kuhakikisha wote wanapata elimu bila ubaguzi.



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema (wapili kulia), akipokea Mwenge wa Uhuru kutoka kwa Mkuu wa Mkoa wa Geita, Rosemary Senyamule, mkoani humo jana, ambapo utakimbizwa kilomita 838 na kupitia miradi 38 kwa kuweka mawe ya msingi na kuzindua. Kulia ni Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa 2022, Sahiri Nyanzabala Geraruma. **PICHA: MARCO MADUHU**

## Wananchi kuondokana matumizi maji machafu

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANANCHI 14,600 wa Mwakitolyo wilayani Shinyanga, wanatarajia kuondokana na adha ya ukosefu wa majisafi na salama, baada ya mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria kukamilika.

Wananchi hao ambao shughuli yao kubwa ni uchimbaji mdogo wa madini ya dhahabu, kwa muda mrefu wamekuwa wakitumia maji yasiyo salama kiafya.

Ahueni hiyo ilibainika juzi wakati Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa, Sahili Nyanzabala Geraruma, alipofika kuweka jiwe la msingi kwenye tangi la mradi wa maji katika kijiji cha Mwakitolyo namba tano.

Mmoja wa wananchi wa eneo hilo, Debora Ngeleja, alisema ukosefu wa majisafi na salama ni tatizo kijiji hapo na kata kwa ujumla kwa sababu maji wanayotumia si salama ikilinganishwa na shughuli zao za uchimbaji wa madini kwa kuwa hutumia zebaki kuchenjulia dhahabu.

"Kukamilika kwa mradi huu wa majisafi na salama utakuwa mkombozi kwetu sisi wananchi wa Mwakitolyo na kuokoa afya zetu na kutotumia tena maji yenye viashiria na mchanganyiko wa kemikali ya zebaki," alisema Ngeleja.

Naye Kiongozi wa Mbio za Mwenge, Geraruma, aliagiza Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kahama na Shinyanga (KASHWASA), kuukamilisha mradi huo kwa wakati pamoja na kuufanyia marekebisho madogo ambayo yamejitokeza.

Alisema ameridhia kuweka jiwe la msingi kwenye mradi huo, huku akitoa maelekezo kuwa mradi huo utakapo kamilika wananchi wavutiwe maji majumbani mwao ndani ya siku saba, ili kuiishi dhana ya kumtua ndoo kichwani mwanamke na siyo kuweka tena vituo vya kuchotea maji.

Aidha, Meneja wa Mradi wa Maji kutoka KASHWASA, Mhandisi Kabigumila Felician, alisema hatua ya mradi ulipofikia ni utandazaji wa mabomba. Alisema tangi la kuhifadhia maji limeshakamilika na mradi huo utahudumia wananchi 14,600 na utagharimu Sh. milioni 272.3.

Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, alisema Mwenge wa Uhuru wilayani Shinyanga utakimbizwa kilomita 102 na utapitia miradi mitano kuweka jiwe la msingi na mingine kuzinduliwa.

# Shirika lasisitiza elimu uzazi watoto wenye vichwa vikubwa

**Na Sabato Kasika**

MKURUGENZI wa Shirika lisilo la Kiserikali la Child Help Tanzania (CHT), Hakim Bayakub, amewataka wadau kuungana kutoa elimu ili kupunguza uzazi wa watoto wenye ulemavu wa vichwa vikubwa na mgongo wazi nchini.

CHT inajishughulisha na utoaji huduma mbalimbali zikiwamo za vifaa tiba kwa watoto wenye ulemavu huo kwa kushirikiana na Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI).

Akizungumza na juzi jijini Dar es Salaam, Bayakub alisema elimu ikitolewa kwa wingi, jamii itaelewa chanzo cha ulemavu huo na kuchukua hatua sahihi za kuuepuka.

"Kwa mfano, tukio la Mei mwaka huu la Sarah Lukelema aliyejinyonga mkoani Njombe, baada ya kujifungua mtoto akiwa na ulemavu huo, asingechukua hatua hiyo kama angekuwa ameelimishwa," alisema Bayakub.

Mkurugenzi huyo alisema umefika wakati sasa wadau wote wanaopiga vita ulemavu huo kuungana na kuzunguka nchi nzima kutoa elimu, hasa maeneo ya vijijini ili kupunguza kasi ya kuwapo kwa watoto wanaozaliwa wakiwa nao.

"Ninaamini kwamba, ukosefu wa elimu kuhusu chanzo cha ulemavu huo ni sababu inayochangia watoto kuzaliwa wakiwa hivyo na pia kuchangia baadhi ya watu wa kujinyonga na wengine kutelekeza familia zao," alisema.

Alisema shirika hilo liko mbioni kuzunguka mikoa mbalimbali, hasa yenye tatizo hilo kwa lengo la kutoa elimu, ambapo aliwataka wadau wengine wakiwamo viongozi wa serikali kushirikiana katika utoaji wa elimu.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, wanaojiandaa kubeba ujauzito wanatakiwa kutumia vidonge vya foliki asidi na vyakula vyenye foliki asidi, ili kuepuka kuzaa watoto wenye ulemavu huo, na kwamba elimu hiyo ikiendelea inaweza kuwa na matokeo chanya.

Ofisa Habari na Mawasiliano wa CHT, Militon Byemerwa, alisema shirika hilo ni mdau mkubwa katika tiba za watoto wenye ulemavu huo, hasa kwenye eneo la ufadhili wa vifaatiba ndani ya taasisi ya MOI ambayo ni mnufaika.

"Tunafadhili mirija ya kuratibu maji ya katika ubongo kwa wenye kichwa kikubwa (shunts), uma za upasuaji kwa wenye mgongo wazi na kichwa kikubwa, mirija ya kusaidia wasio na hisia za haja kubwa na ndogo (catheters)," alisema Byemelwa.

Katika ufafanuzi wake, alisema mirija hiyo ni maalum ambayo inahakikisha maji hayawi mengi kichwani, kwa kuwa yakiwa mengi kinaweza kuongezeka, hivyo wanajitahidi kuhakikisha huduma hiyo inapatikana.

Alisema, Child Help Tanzania inatoa elimu kwa umma kuhusu kinga ya tatizo hilo na matibabu yake, lengo likiwa ni kuona jamii yenye afya bora bila ulemavu wa kichwa kikubwa na mgongo wazi.

"Kimsingi tukio la mwanamke aliyejinyonga kwa sababu ya kuzaa mtoto mwenye kichwa kikubwa na mgongo wazi lilitugusa tukaamua kusafiri hadi Njombe kwa ajili ya kuchukua mtoto wa marehemu na kumpeleka kwa madaktari wa MOI,"alisema.

Byemelwa alisema, shirika linatamani kuhakikisha kila mwenye ulemavu huo awe mtoto au mtu mzima, wanapata huduma zote za kiafya, lakini watu wazima wakiajiriwa bila kubaguliwa kutokana na ulemavu huo.

# THE MWALIMU NYERERE MEMORIAL ACADEMY

## VACANCY ANNOUNCEMENT

**1.0 Introduction**

The Governing Board of the Mwalimu Nyerere Memorial Academy seeks to recruit two Deputy Rectors (Academic, Research and Consultancy & Planning, Finance and Administration) and the Director for MNMA Zanzibar Campus from suitably qualified and competent Tanzanians with excellent credentials.

**2. Qualifications and Experience**

**2.1 DEPUTY RECTOR ACADEMIC, RESEARCH AND CONSULTANCY**

**a. Qualifications and Experience**

The applicant must be a holder of a PhD Degree (NTA Level 10 or equivalent) in any field offered by the Mwalimu Nyerere Memorial Academy and should be at least a Senior Lecturer. Be a person with outstanding academic, administrative experience and capability in the area of technical education and training. The applicant must have work experience of at least ten (10) years of which at least two (2) years should be served at a Managerial level.

**b. Duties and Responsibilities**

i. To assist the Rector in all matters relating to academic functions of the Academy;
ii. To facilitate learning by teaching of academic programmes at the Academy;
iii. To ensure smooth operation and development of academic matters of the Academy;
iv. To establish and maintain a workable system for regular monitoring and evaluation and the performance, quality, relevance and efficiency of all academic programmes;
v. To review existing academic programmes and develop new ones based on the established needs and market signals;
vi. To plan, promote and advise the Rector on admissions, examinations and students' policies and procedures;
vii. To assist the Rector in promoting efficiency in training, research and consultancy services;
viii. To prepare and control curricula; and
ix. To perform any other official duties as may be assigned by the immediate supervisor.

**c. Salary Scale**

As per substantive post salary scale

**d. Tenure of Office**

The Deputy Rector for Academic, Research and Consultancy shall hold office for a term of four years (4) and may be re-appointed consecutively for one more term of four (4) years.

**2.2 DEPUTY RECTOR PLANNING, FINANCE AND ADMINISTRATION**

**a. Qualifications and Experience**

The applicant must be a holder of a PhD Degree (NTA Level 10 or equivalent) in any field offered by the Mwalimu Nyerere Memorial Academy and should be at least a Senior Lecturer. Be a person with outstanding academic, administrative experience and capability in the area of technical education and training. The applicant must have work experience of at least ten (10) years of which at least two (2) years should be served at a Managerial level.

**b. Duties and Responsibilities**

i. To assist the Rector in all financial, human resources and administrative matters of the Academy;
ii. To conduct a review of existing and develop new physical, financial, accounting, human resources and administrative programmes based on established needs of the Academy;
iii. To formulate manpower planning and development of Academy's employees;
iv. To plan and control all financial and accounting operations of the Academy;
v. To be a recorder to the Governing Board Meetings;
vi. To be a custodian of the Academy Seal;
vii. To coordinate preparation of budget and final accounts;
viii. To safe guard and use of Academy Assets such as machines and vehicles;
ix. To supervise and deal with disciplinary matters of staff in the Academy in accordance with the laid down rules and regulations;
x. To. develop staff training programme of the Academy and deal with staff development and training; and
xi. To perform any other official duties as may be assigned by the immediate supervisor.

**c. Salary Scale**

As per substantive post salary scale

**d. Tenure of Office**

The Deputy Rector for Planning, Finance and Administration shall hold office for a term of four years (4) and may be re-appointed consecutively for one more term of four (4) years.

**2.3 CAMPUS DIRECTOR FOR MWALIMU NYERERE MEMORIAL ACADEMY, ZANZIBAR CAMPUS**

**a. Qualifications and Experience**

The applicant must be a holder of PhD Degree (NTA Level 10 or equivalent) from a recognized Higher Learning Institution in any field relevant to the Mwalimu Nyerere Memorial Academy. Must have a post PhD extensive teaching experience of not less than three (3) years in an accredited Higher Learning Institution.

**b. Duties and Responsibilities**

i. To be the In-charge of the MNMA Zanzibar Campus and reporting to the Rector of Mwalimu Nyerere Memorial Academy;
ii. To be responsible for proper administration of the MNMA Zanzibar Campus in accordance with the policy laid down by the Governing Board;
iii. To be responsible for the enforcement of by-laws and regulations made by the Governing Board;
iv. To be responsible for exercising such other functions and powers as are conferred on him/her by the Governing Board or by the Mwalimu Nyerere Memorial Academy Act No. 6 of 2005 and its amendments;
To be responsible for promoting good relations with the Government and other organizations; vi. To be responsible for promoting efficiency in the academic activities related to training, research and consultancy; and
vii. To perform any other official duties as may be assigned by the immediate supervisor.

**c. Salary Scale: As per substantive post salary scale.**

**d. Tenure of Office:**

Campus Director shall hold office for a term of four (4) years and may be re-appointed consecutively for one more term of four years.

**3. Mode of Application**

- Applications should be submitted with the copies of an up - to - date and detailed curriculum vitae (detailing academic qualifications, publications, awards/scholarship/funding membership to professional associations and linkages), copies of relevant certificates, e-mail addresses, telephone contacts and at least one reference letter.
- Applications should be addressed to the email "cnpallangyo@gmail.com" and copy to "prucheria.rwehambura@mnma.ac.tz" titled "Application for the Position of Deputy Rector Academic, Research and Consultancy" or "Application for the Position of Deputy Rector for Planning, Finance and Administration" or Application for the Position of the Campus Director - Karume Campus - Zanzibar.
- Only short-listed candidates shall be notified and shall be required to make themselves available for interaction at an appointed place and date.
- Deadline for submitting applications is **5th August, 2022**

All applications should be addressed to the following address;

**The Chairperson,**

**Search Committee for the Deputy Rectors and the Director of Mwalimu Nyerere Memorial Academy, Zanzibar Campus,**
Email (**cnpallangyo@gmail.com**; **prucheria.rwehambura@mnma.ac.tz**)
**Mobile: +255757604499**

**Issued by:**

**Rector,**
**Mwalimu Nyerere Memorial Academy,**
**P.O. Box 9193**
**Dar es Salaam.**

216962702

Access Microfinance Bank Tanzania

# UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA ZISIZOKAGULIWA KWA UMMA

Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 JUNI 2022

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | (Kiasi kwa shilingi milioni) | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Robo ya Mwaka sasa 30 JUNI 2022 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30 JUNI 2021 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30 JUNI 2022 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30 JUNI 2021 |
| 1 Mapato ya Riba | 4,885 | 3,884 | 9,421 | 7,605 |
| 2 Gharama za Riba | (797) | (656) | (1,453) | (1,325) |
| 3 Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2) | 4,088 | 3,228 | 7,968 | 6,280 |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | - | 0 | - | - |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (660) | (368) | (1,270) | (1,097) |
| **6 Mapato Yasiyo ya Riba:** | **1,063** | **755** | **1,991** | **1,384** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 11 | 35 | 24 | 75 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 361 | 244 | 634 | 477 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | 691 | 476 | 1,332 | 832 |
| **7 Gharama Zisizo za Riba:** | **(3,955)** | **(3,121)** | **(8,366)** | **(7,030)** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | (2,667) | (2,179) | (5,374) | (3,963) |
| 7.2 Ada na Kamisheni | (137) | (139) | (267) | (305) |
| 7.3 Gharama Nyingine | (1,152) | (803) | (2,725) | (2,762) |
| **8 Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **535** | **494** | **322** | **(463)** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | (24) | - | (24) | - |
| **10 Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **511** | **494** | **298** | **(463)** |
| 11 Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | - | - | - | - |
| **12 Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **511** | **494** | **298** | **(463)** |
| 13 Idadi ya Waajiriwa | 401 | 329 | 401 | 329 |
| 14 Mapato kwa Hisa | 51 | 49 | 30 | (23) |
| 15 Idadi ya Matawi | 8 | 8 | 8 | 8 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 3.23% | 3.22% | 0.97% | -1.50% |
| (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 31.82% | 30.90% | 9.39% | -13.40% |
| (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 66.49% | 67.27% | 73.31% | 78.21% |
| (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 38.46% | 33.32% | 39.11% | 31.78% |

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 JUNI 2022


(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | (Kiasi kwa shilingi milioni) | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Robo Mwaka ya sasa 30 JUNI 2022 | Robo Mwaka iliyopita 31 MACHI 2022 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30 JUNI 2022 | Limbikizo la robo Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30 JUNI 2021 |
| **I: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | 535 | (213) | 322 | (463) |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | |
| - Hasara Katika Mali | 930 | 878 | 1,808 | 600 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (4,469) | (2,240) | (6,952) | (551) |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 5,141 | 559 | 5,190 | (3,581) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | (159) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (353) | (748) | (749) | 604 |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 512 | (958) | (45) | (1,252) |
| - Kodi Iliyolipwa | (73) | (73) | (146) | (41) |
| - Mengineyo (bainisha) | (236) | (35) | (271) | 184 |
| *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji* | **1,989** | **(2,830)** | **(842)** | **(4,659)** |
| **II: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (55) | (26) | (81) | - |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | 10 |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mapato ahirishwa | (18) | (16) | (34) | (33) |
| *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | **(74)** | **(42)** | **(116)** | **(23)** |
| **III: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha | - | - | - | - |
| | | | - | - |
| **IV: Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | **1,915** | **(2,872)** | **(958)** | **(4,682)** |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Kipindi | **6,703** | **9,575** | **9,575** | **17,864** |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Kipindi | **8,618** | **6,703** | **8,618** | **13,182** |

## TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 JUNI 2022

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | (Kiasi kwa shilingi milioni) | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Jumla |
| **Kipindi cha sasa hadi 20 JUNI 2022** | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka 2022 | 40,000 | - | (34,166) | 581 | - | 6,416 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 298 | - | - | 298 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | 369 | (369) | - | - |
| **Salio la mwisho wa 30 Juni 2022** | **40,000** | **-** | **(33,499)** | **212** | **-** | **6,714** |
| **Kipindi cha Mwaka uliopita hadi 30Juni 2021** | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka 2021 | 40,000 | - | (35,570) | 2,709 | - | 7,139 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (463) | - | - | (463) |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | 1,991 | (1,991) | - | - |
| **Salio la mwisho wa 30 Juni 2021** | **40,000** | **-** | **(34,042)** | **718** | **-** | **6,676** |




## WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 JUNI 2022

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | (Kiasi kwa shilingi milioni) | |
|---|---|---|---|
| | | Robo Mwaka ya sasa 30 JUNI 2022 | Robo Mwaka iliopita 31 MACHI 2022 |
| **A.** | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 6,093 | 4,600 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 4,165 | 4,491 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | - | - |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 1,016 | 319 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 60 | 60 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | - | 464 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 44,204 | 39,735 |
| 12 | Mali Nyingine | 8,737 | 9,250 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 963 | 1,019 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **65,237** | **59,939** |
| **B.** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 1,500 | 1,000 |
| 18 | Amana za Wateja | 47,914 | 43,272 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 1,227 | 1,299 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 1,894 | 1,879 |
| 27 | Dhima Nyingine | 5,989 | 6,285 |
| 28 | Madeni | - | - |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **58,524** | **53,736** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI *(16 kutoa 29)*** | **6,714** | **6,203** |
| **C.** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 40,000 | 40,000 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | - | - |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (33,797) | (33,904) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 298 | (213) |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 212 | 320 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **6,714** | **6,203** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 1,018 | 1,018 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 5,694 | 6,156 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 4,956 | 5,019 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | 64 | 64 |
| **D.** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 10.29% | 10.35% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 11.58% | 13.75% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 99.49% | 101.09% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 67.76% | 66.29% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 67.76% | 67.07% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 11.61% | 3.65% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 8.84% | 0.70% |

**BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 JUNI 2022**

Katika kuanda taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita.

| Jina | Cheo | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| Julius Justine Ruwaichi | Offisa Mtendaji Mkuu | imesainiwa | 23 Julai 2022 |
| Tajinder Singh Bhachu | Kaimu Mkuu wa Fedha | imesainiwa | 23 Julai 2022 |
| Catherine Temu | Mkaguzi Mkuu wa Ndani | imesainiwa | 23 Julai 2022 |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

| **Jina** | **Cheo** | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| Mr.Thomas Engelhardt | Mwenyekiti | imesainiwa | 23 Julai 2022 |
| Mr. Johannes Mainhardt | Mkurugenzi | imesainiwa | 23 Julai 2022 |

21696250 1

## TANGAZO

Access Microfinance Bank Tanzania

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amsema azma ya serikali ni kujenga shule ya msingi ya ghorofa katika kisiwa cha Kojani ili kuendana na mahitaji yaliyoko.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana baada ya kuweka jiwe la msingi la madarasa saba yaliyojengwa na Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo Zanzibar (KMKM) huko Kojani, Wete Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Aliwaahidi wananchi wa kisiwa cha Kojani kujenga shule hiyo ya ghorofa ya msingi katika kisiwa hicho kutokana na idadi ya wanafunzi kuwa kubwa.

Sambamba na hayo, Rais Dk. Mwinyi alisema serikali itaendelea na ujenzi wa madarasa matano yaliyobaki katika eneo hilo huku akitumia fursa hiyo kumpongeza Sheha wa Kojani kwa uchapakazi wake mzuri ikiwa ni pamoja na kutoa ardhi yake kwa kujenga skuli hiyo.

Rais alitumia fursa hiyo kutoa pongezi kwa kikosi cha KMKM kwa kujenga madarasa saba ndani ya mwezi mmoja.

Alisema hatua zitakazochukuliwa na serikali katika kuwasaidia wavuvi wadogo na kueleza hatua zitakazochukuliwa katika kuhakikisha wanafikia malengo yaliyokusudiwa ikiwa ni pamoja na kupeleka maboti kisiwani humo.

Pia Rais Dk. Shein aliahidi kwamba serikali itaitafutia ufumbuzi changamoto ya majisafi na salama kupitia Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA).

Kwa upande wa sekta ya afya, Rais Dk. Mwinyi aliutaka uongozi wa Wizara ya Afya kulitafutia ufumbuzi suala la wahudumu wa kituo cha afya.

Pamoja na hayo, Rais Dk. Mwinyi aliyapongeza mapokezi makubwa aliyoyapata kutoka kwa wananchi wa kisiwa cha Kojani na kueleza jinsi alivyofarijika.

Naye Mke wa Rais wa Zanzibar, Mama Mariam Mwinyi, aliwasisitiza wanafunzi wa Kojani kusoma kwa bidii ili waweze kupata mafanikio makubwa zaidi hapo baadaye.

Mkuu wa Kikosi Maalum cha KMKM, Komodo Azana Hassan Msingiri, alieleza changamoto walizozipata katika ujenzi huo na kusisitiza kwamba hatua za makusudi walizichukua katika kuhakikisha ujenzi huo unafanikiwa na ndio maana wakajenga madarasa hayo saba kwa mwezi mmoja.

Mapema, Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Ali Khamis, alisema ujenzi wa madarasa hayo ya Shule ya Msingi Kojani unajumuisha madarasa saba ambao ni miongoni mwa madarasa yanayojengwa kupitia programu ya UVIKO-19.

Alisema serikali imeamua kujenga skuli hiyo katika eneo hilo kutokana na kutokuwapo kwa eneo la kutosha katika shule kongwe ya Kojani ambayo kwa sasa imezungukwa na makazi ya wananchi.

Alisema kwa sasa shule hiyo ina wanafunzi wapatao 2,257 msingi na maandalizi kwa vyumba 16 vya kusomea wastani wa wanafunzi 70 kwa chumba kimoja kwa utaratibu wa kusoma mikondo miwili yaani asubuhi na jioni.




Mke wa Rais wa Zanzibar, Mama Mariam Mwinyi (kulia), akiwasalimia wakazi wa Kojani, wakati wa hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi la ujenzi wa Shule ya Msingi Kojani, Pemba jana, inayojengwa kwa fedha za Uviko-19. **PICHA: IKULU**

# Neema kiwanda kipya cha maji

**Na Rahma Suleiman,** PEMBA

AZMA ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, kukifanya Kisiwa cha Pemba kuwa cha viwanda imeanza kuonekana baada ya kuzindua kiwanda cha maji eneo la Chamanangwe kisiwani hapo.

Akizungumza baada ya kuzindua kiwanda hicho juzi, Dk. Mwinyi alisema serikali imetenga eneo la Chamangwe kuwa mahsusi kwa uwekezaji wa viwanda, likiwa na ukubwa wa hekta 136.

Alisema uwekezaji katika Kisiwa cha Pemba umepata baraka kubwa katika kipindi cha miaka miwili kufuatia kuimarika kwa mazingira ya amani na utulivu.

Dk. Mwinyi alisema kutokana na kuimarika kwa mazingira ya amani na utulivu, sasa kuna mategemeo makubwa ya kufikia malengo ya kuzalisha ajira 300,000 zilizoahidiwa na Chama Cha Mapinduzi kupitia Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2020-2025.

"Nilipoingia madarakani, nilisema ninakwenda kukifungua Kisiwa cha Pemba kwa uwekezaji wa miradi mbalimbali katika sekta ya viwanda. Sasa ile ndoto imeanza kutimia katika uwekezaji eneo la viwanda Chamanangwe, Pemba," alisema.

Dk. Mwinyi alizitaka taasisi mbalimbali zinazofanya kazi katika uwekezaji, likiwamo Shirika la Umeme (ZECO), kujipanga kuzipatia ufumbuzi kero za upatikanaji wa nishati ya umeme katika kipindi cha miaka mitano.

Alisema mikakati iliyoko ni kuongeza kiwango cha umeme kutoka megawati 20 ambazo haziwezi kuendesha shughuli za uwekezaji wa miradi ya viwanda.

Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Omar Said Shaaban, alisema hakuna vikwazo kwa wawekezaji wa bidhaa mbalimbali za viwanda kutoka Zanzibar kuingia katika Soko la Tanzania Bara lenye mahitaji makubwa ya watu.

Alisema kero zilizojitokeza awali za kibiashara kati ya Tanzania Zanzibar na Tanzania Bara tayari zimepatiwa ufumbuzi na pande mbili za serikali.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga, alisema jumla ya wawekezaji watano wamejitokeza kuwekeza katika eneo hilo la viwanda la Chamanangwe.

Alisema tayari ujenzi wa kiwanda cha kusarifu na kuongeza thamani katika zao la mwani umeanza, hivyo kuwa neema kwa wakulima wake, ambao kwa asilimia 80 ni wanawake.

Alivitaja viwanda vingine vinavyotarajiwa kujengwa ni pamoja na cha mabati kinachotarajiwa kujengwa na Kampuni ya Sakina Group na vya mabomba ya maji na mafuta ya kula, hatua aliyoitaja itasaidia kuongeza ajira kwa vijana.

"Uwekezaji katika Kisiwa cha Pemba katika kipindi cha miaka mitano unatarajiwa kufikia dola bilioni moja pamoja na ukodishwaji wa visiwa vitano," alisema.

Mwekezaji wa kiwanda cha maji kilichozinduliwa, Husamodin Ali, alisema kuwa kikwazo kikubwa kwao ni shida katika upatikanaji wa umeme, akifafanua kuwa uliopo sasa hauna nguvu kwa kuwa kiwanda hicho pekee kinatumia megawati 12.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA KAGERA**
**LILILOPO BUKOBA.MAOMBI NA 37/2022**
**DHIDI YA**
**1.HONORATUS RWEBUGISA**
**2.WILLBROAD MWOMBEKI RWEBUGISA............WAOMBAJI**
**DHIDI YA**
**FORTUNATUS MPANGAMILA .........MJIBU MAOMBI**

**KWA FORTUNATUS MPANGAMILA**
**(POPOTE PALE ULIPO)**

Unaarifiwa kuwa maombi na 37/2022 yamepangwa kutajwa tarehe 5.09.2022 mbele ya Mwenyekiti wa Baraza PJ Makwandi saa 2.00 asubuhi
Hivyo unaamuriwa kuhudhuria wewe mwenyewe/mwakilishi wako mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.Msipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja dhidi yako na hukumu kutolewa.
**AMRI** hii imetolewa kwa mkono wangu na MHURI wa Baraza hili leo **tarehe 19.7.2022**

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA
BUKOBA

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI SHAHIDI**
**(MCA/63)**
**MAHAKAMA YA MWANZO YA KIBITI**
**WILAYA YA KIBITI**
**MADAI NAMBA 11...2022**
**MDAI: GILBERT MUSHI (CARBON PLANT LTD)**
**MADAI**
**MDAIWA: MC WATER WELLS DRILLING PLUMBING**
**KWA: MOHAMED SAID MGOMBA**
**D'SALAAM**

Kwa kuwa mdai / wadai ameleta / wameleta madai yake / yao kwamba ( Eleza hapo habari za mdai ) **MADAI YA FEDHA KIASI CHA TSH. 11,000,000/=( MILIONI KUMI NA MOJA TU) AMBAZO MLILIPWA KWAAJILI YA KUCHIMBA KISIMA NA KAMPUNI YA CARBON PLANET LTD.**
Kwa hiyo unahitajiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya **JUMATANO** tarehe 10-08-2022 saa 2.30 Asubuhi kwa kujibu madai hayo,na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwajili ya kujitetea katika shauri hilo.

**ANGALIA** Kama hukuhudhuria/hamkuhuzuria siku iliyotajwa hapo juuu.Mahakama ikithibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shauri hii, itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa Amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe **15 JULAI 2022**.

**Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo**

---

**MAHAKAMA YA WILAYA YA MIRATHI NYAMAGANA MWANZA**

**SHAURI LA MIRATHI NO.17/2022**

**MWOMBAJI.........................JAPHET E. J. NYALAJA**

**MAREHEMU...........JACKSON NYALAJA MAHANDE**

**KWA: YEYOTE ANAYEHUSIKA**

**KUITWA SHAURINI**

Mwombaji tajwa hapo juu amefungua shauri la mirathi ya marehemu **JACKSON NYALAJA MAHANDE** katika Mahakama hii, hati za mirathi zinapatikana katika mahakama hii.

Yeyote mwenye pingamizi katika mirathi hii anatakiwa kuweka pingamizi lake siku ya kesi hapa Mahakamani tarehe 3/8/2022 kutolewa kwa tangazo hili.

Imetolewa kwa mkono wangu na muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 20/07/2022.

HAKIMU MKAZI
WILAYA YA NYAMAGANA
MWANZA

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JACQUELINE DEOGRATIAS** RUTATORA anatangaza kupotelewa na kadi yake ya gari yenye namba za usajili **T 725 BJN.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Taarifa ya polisi:
**DSM/PHQ/RB/295597/2022.**

---

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

---

**NGOMENI ENTERPRISES**

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA NA NOTISI YA KULIPA DENI

Kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na crdb bank makao makuu Dar es salaam tunatoa notisi ya siku nne (14) tu ili uweze kulipa deni lako lote unalodaiwa na CRDB Bank pamoja na gharama za Dalali. Kukaidi au kushindwa kulipa deni hilo tutauza dhamana uliyoweka kwa mnada wa hadhara kama inavyoonesha kwenye jedwari hapo chini.

| S/N JINA LA MDAIWA | DHAMANA MAHALI | TAREHE/MUDA |
|---|---|---|
| Edson Brighton Bebwa | Kizinga -Majohe Area Block D, Plot no. 122-Ilala | 11.08.2022 saa 2 asubuhi na kuendelea |
| Nuru Omari Muhaji | Goba -Kunguru Area Block c , Plot no, 2427 | 13.08.2022 saa 2 asubuhi na kuendelea |
| Jamal S. Makomelo | Ifakara town -uwanja wa Taifa "B' Viwanja sitini area | 15.08.2022 saa 2 asubuhi na kuendelea |

**MASHARTI YAMNADA.**

1. Dhamana itauzwa kama zilivyo.
2. Mnunuzi atakayeshinda atalipa malipo ya awali ya asilimia 25 ya bei itakayofikiwa siku ya mnada na asilimia 75 atalipa ndani ya siku 14.
3. Mnunuzi atakayeshindwa kumalizia salio la asilimia 75 katika muda uliopangwa hapo juu, hatarudishiwa fedha alizolipa awali na mnada utarudiwa siku nyingine itakayopangwa.
4. Gharama zote za kubadilisha hati miliki, kutwaa nyuma na gharama nyinginezo zitakuwa juu ya mnunuzi.
5. Wateja wote mnakaribishwa kuona na kukagua nyumba muda wote isipokuwa usiku.

**MAWASILIANO:**
**CRDB BANK PLC, HEAD QUARTER.**
**NGOMENI ENTERPRISES, DSM.**
**SIMU: 0719974916/ 078425204**

---

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie: 0782253676**

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710. E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Ulaya wakubaliana njia endapo gesi itasitishwa

**BERLIN, Ujerumani**

NCHI wanachama wa Umoja wa Ulaya, zimekubaliana kuhusu mpango wa dharura wa kukabiliana na athari zinazoweza kusababishwa na hatua ya Russia kusitisha usafirishaji wa gesi. Wanadiplomasia wameliambia shirika la habari la Ujerumani (DPA), kwamba mpango huo unaainisha punguzo la asilimia 15 la matumizi ya gesi asilia kwa hiari katika nchi wanachama kati ya Agosti mosi mwaka huu na Machi 31 mwaka ujao.

Pia mkakati utawekwa kutoa tahadhari katika maeneo yote ya umoja huo iwapo kutatokea uhaba mkubwa wa gesi na kutekeleza malengo ya uhifadhi yenye mafungamano.

Chini ya makubaliano hayo mapya yaliyofanyiwa marekebisho, viwango vya uhifadhi vyenye mafungamano vinaweza kutekelezwa na baraza la Ulaya badala ya kamisheni ya Umoja wa Ulaya. Hapo jana kampuni ya nishati ya Russia, Gazprom ilitangaza itapunguza usafirishaji wa gesi hadi Ujerumani kupitia bomba la gesi la Nord Stream 1 kutoka asilimia 40 ya uwezo wake jumla hadi asilimia mbili.

Lavrov aitembelea Uganda

Katika hatua nyingine, Waziri wa Mambo ya Nje wa Russia, Sergei Lavrov mefanya mazungumzo na rais wa Uganda Yoweri Museveni.

Hayo ni kwa mujibu wa shirika la habari la Russia (TASS). Lavrov aliwasili nchini humo katika kituo chake cha tatu cha ziara yake barani Afrika.

Msemaji wa wizara ya mambo ya nchi za nje ya Russia, Maria Zakharova alisema Lavrov alilakiwa mjini Entebbe na waziri mwenzake wa Uganda, Jeje Odongo.

Maofisa wa Uganda hawajatoa taarifa zaidi kuhusu ratiba ya Lavrov nchini humo, lakini serikali ilisema siku ya Jumapili kwamba ziara ya mwanadiplomasia huyo itakuwa ya siku mbili.

Ziara ya Lavrov barani Afrika ilianzia mjini Cairo ambako aliwahakikishia viongozi wa Misri kwamba mahitaji yao ya nafaka kutoka Russia yatashughulikiwa na kutimizwa.

Lavrov aliwasili Kampala akitokea Brazzaville, Jamhuri ya Congo na anatarajiwa kuitembelea pia Ethiopia. *DW*

## China yatoa onyo kali kwa Marekani

**TAIPEI, Taiwan**

WIZARA ya Mambo ya Nje ya China, imetoa onyo zito kwa Spika wa Marekani, Nancy Pelosi ambaye ameitembelea Taiwan.

Taarifa ya wizara hiyo iliyochapishwa katika gazeti la Financial Times, yenye kichwa ha habari ''Beijing yatoa onyo kali zaidi kwa Washington, ilisema itachukua hatua kali kama nchi hiyo inapuuzia onyo hilo.

China ilisema iwapo Marekani haitazingatia onyo hilo, itachukua hatua kali japo haikusema kama hatua hiyo ni ya kijeshi.

Msemaji wa wizara hiyo, Zhao Lijian alisema Washington inataka kufafanua msimamo wake kuhusu Taiwan.

Ikulu ya White House ilikataa kujibu onyo hilo la China.

Serikali ya Taiwan ilisema kwamba mustakabali wa kisiwa hicho utaamuliwa na watu milioni 23 wanaoishi katika kisiwa hicho.

**BBC**

## Wachunguzi wa haki za binadamu wa Umoja wa Mataifa wazuru Ethiopia

TUME ya Umoja wa Mataifa iliyopewa kibarua cha kuchunguza ukiukaji wa haki za binadamu uliofanywa wakati wa vita katika eneo la Tigray, nchini Ethiopia, inaendelea na ziara yake iliyoanza juzi.

Baraza la haki za binadamu la Umoja wa Mataifa liliiunda tume hiyo mnamo Desemba mwaka uliopita kwa muhula wa mwaka mmoja unaoweza kurefushwa kuchunguza vitendo vya kinyume cha sheria za kimataifa za haki za binadamu, sheria kuhusu ubinadamu na sheria kuhusu wakimbizi.

Hata hivyo, serikali ya Ethiopia ilitoa taarifa ikisema ingetafakari upya uamuzi wake kushirikiana na tume hiyo kulingana na jinsi itakavyofanya kazi na ikiwa itauheshimu msimamo wa serikali.

Shirika la habari lililo karibu na serikali Fana BC, liliripoti kwamba wachunguzi hao wa Umoja wa Mataifa walikutana na Waziri wa Mambo ya Nje wa Ethiopia, Demeke Mekonnen.

Wataalamu wa tume hiyo walikuwa mjini Addis Ababa juzi kwa mazungumzo na maofisa wa serikali na wadau wengine kuhusu kanuni na masharti ya ushirikiano. **DW**



Watoto wakisimama juu ya mtumbwi ambao umekwama juu ya matope yaliyokauka kutokana na jua kali kusini mwa Chibayish katika jimbo la Qar nchini Iraq. **PICHA: AFP**

# UN yatabiri Libya haitatawalika

**NEWYORK, Marekani**

OFISA mwandamizi wa Umoja wa Mataifa, amesema Libya inakabiliwa na mkwamo wa kisiasa na kikatiba uliosababisha ongezeko la mapigano, hali ngumu ya kiuchumi na maandamano yanayofanywa na raia waliokata tamaa.

Naibu Katibu Mkuu, Marth Pobee alikiambia kikao cha baraza la usalama la Umoja wa Mataifa juzi kwamba hali ya jumla nchini humo inabaki kuwa tete huku hali ya wasiwasi ya usalama na machafuko yanayofanywa na makundi ya waasi yanayojihusisha katika mchakato wa kisiasa yakishuhudiwa.

Pobee amezihimiza nchi wanachama wa baraza la usalama na washirika wa kimataifa wa Libya kutumia ushawishi wao kuwaraia mahasimu wakubaliane kuandaa uchaguzi haraka iwezekanavyo.

Balozi wa Libya katika Umoja wa Mataifa, Teher El Sonni alisema hali ya sasa huenda ikazidi kuwa mbaya kiasi cha kutodhibitika kama hakutapatikana suluhisho mbali na uingiliaji kati wa mataifa ya kigeni na michakato ya kisiasa.

*DW*

# Zimbabwe yazindua sarafu za dhahabu

**HARARE, Zimbabwe**

BENKI Kuu ya Zimbabwe imezindua sarafu mpya ya dhahabu katika juhudi za kukabiliana na ongezeko la mfumuko wa bei na kushuka kwa sarafu ya nchi hiyo.

Kiwango kikuu cha riba cha benki kuu kiliongezeka zaidi ya mara mbili mwezi huu hadi kufikia asilimia 200 baada ya kiwango cha mfumuko wa bei kupanda zaidi ya silimia 190

Kila sarafu itawekwa bei kwa kiwango cha soko la kimataifa kwa wakia moja ya dhahabu pamoja na asilimia tano kama gharama za uzalishaji.

Kufikia Ijumaa ya wiki iliyopita, wakia moja ilikuwa na thamani ya dola 1,724.

Hata hivyo,itawezekana kutumia sarafu hizo madukani, ikiwa zitakuwa na chenji ya kutosha, hayo ni kwa mujibu wa gavana wa Benki Kuu ya Zimbabwe, John Mangudya.

Sarafu hiyo inaitwa "Mosi-oa-Tunya" ambayo ina maana ya "Moshi Unaounguruma" na ina picha ya maporomoko ya maji ya Victoria, kwenye mpaka kati ya Zimbabwe na Zambia.

*BBC*

# BONDIA KIDUNDA ATUA SONGEA, AAHIDI KUMCHAPA KATOMPA

**Na Saada Akida**

BONDIA wa ngumi za kulipwa nchini, Seleman Kidunda tayari amewasili mjini Songea kumkabili mpinzani wake, Tshimanga Katompa kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) katika pambano la kimataifa kuwania mkanda wa ubingwa wa Dunia wa WBF.

Pambano hilo lililopewa jina la Pay Back Night linatarajiwa kufanyika Jumamosi hii katika uwanja wa Majimaji, Songea mkoani Ruvuma.

Kidunda aliwasili juzi mkoani humo na kupokelewa na wazee wa kimila wa mjini hapa, walimsimika kwa kumvalisha mavazi ya rangi nyekundu na shada ikiwa ni ishara ya kumtambua kama shujaa wao mkoani hapo, kabla ya msafara kutoka uwanja wa ndege na kuelekea makumbusho ya vita ya majimaji.

Katika msafara huo, Kidunda alipita maeneo mbalimbali na kila alipokuwa akisimama alitoa ahadi kubwa ya kumchapa Katompa ndani ya mkoa huo alipozaliwa. Wazee hao wakimila waliongozwa na Chifu, Yusuph Mbano ambaye amemsimika kama shujaa wao kabla ya msafara wake kukatisha katika mitaa mbalimbali mjini hapa na kuelekea kwenye makumbusho ya vita ya majimaji, aliweka shada la maua katika kaburi moja walikozikwa mashujaa 66 walionyongwa na utawala wa kikoloni wa Ujerumani.

Chifu Mbano alisema kwa upande wao washatimiza wajibu wao kwa kuweza kumtambua bondia huyo kwa kuwa ni kijana wao, wanaamini atashinda pambano na kuweza kuheshimisha nchi kimataifa.

Kidunda amewashukuru kwa kuwaambia anatambua mzigo mkubwa uliokuwa mbele yake, lakini akiwa ni kijana aliyezaliwa mkoa wa Ruvuma naamini hatoweza kuwaangusha kwa kumchapa mpinzani wake huku akiwasisitiza wajitokeze kwa wingi kushuhudia ngumi biliani.




Bondia wa ngumi za kulipwa nchini, Seleman Kidunda akiwa juu ya gari akiwapungia mashabiki wakati akizunguka kwenye mitaa ya mji wa Songea, juzi. **PICHA: SAADA AKIDA**

# Nyoni atoa tahadhari Ligi Kuu

**Na Saada Akida**

BEKI Mkongwe wa Simba, Erasto Nyoni ametoa tahadhari kwa wapinzani wake kujipaanga vizuri kwani wamedhamiria kufanya kweli kupigania kurejesha mataji yote matatu kwa msimu wa 2022/23.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nyoni alisema msimu uliopita haukuwa mzuri kwao kwa sababu hawakufikia malengo yao na sasa wachezaji hawataki kuona makosa yake yanajirudia.

Alisema msimu uliopita haukuwa na mafanikio kwani walipoteza kila kitu na ilikuwa kumbukumbu mbaya zaidi kukubali kupoteza mechi mbili kwa watani wao wa jadi (Yanga).

"Msimu ujao utakuwa mgumu sana, tunaona timu zinavyosajili kikubwa wajipange kwa sababu tunakuja kivingine kuhakikisha tunatwaa mataji yetu matatu tukianza na Ngao ya Jamii," alisema Nyoni.

Alisema ameangalia usajili unaofanywa na timu yake na ana imani wakijitoa na kujituma watafikia malengo yao ya kuhakikisha wanawapa furaha mashabiki wa Simba na kurejesha heshima ya klabu hiyo katika michuano yote.

"Kuhusu ushindani wa namba ndani ya kikosi ni mkubwa sana, ukizingatia sajili ambazo zinafanywa na viongozi wetu kuimarisha madhaifu ya kikosi chetu na kufanya vizuri katika michezo ijayo," alisema Nyoni.

Simba iko kambini, mji wa Ismailia nchini Misri kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya, utakaofunguliwa Agosti 13 mwaka huu kwa mchezo wa Ngao ya Jamii dhidi ya Yanga, utakaopigwa katika uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

## Mlipili asajiliwa Prisons, ikiacha 10

**Na Adam Fungamwango**

BEKI wa zamani Simba, Yusuph Mlipili amejiunga na klabu ya Prisons, akitokea Singida Big Stars.

Taarifa iliyotolewa na Idara ya Habari na Mawasiliano ya klabu hiyo imesema beki huyo ambaye aliichezea timu hiyo kwenye Ligi ya Championship ikiitwa DTB, amejiunga na Maafande hao na kuwa mchezaji wa kwanza msimu huu kusajiliwa.

"Hivi ndivyo tunavyoanza, Mlipili ni wa kijani na nyeupe." Uliandika mtandao rasmi wa klabu hiyo mara baada ya kukamilisha usajili huyo.

Mlipili ambaye ni beki wa kati, aliichezea Simba 2017 akitokea Toto African, hadi 2020 alipoondoka kwenda kujiunga na Kagera Sugar.

Wakati Prisons ikianza rasmi usajili, imewapa mkono wa kwaheri wachezaji wake 10 kwa sababu mbalimbali ikiwemo utoro na kushuka kwa viwango.

Wachezaji walioachwa ni Mohamed Mkopi, Adili Buha, Salum Upuu, Gwamaka Bangu, Hassan Mshamu, Julius Kwanga, Lambart Sabianka kwa matatizo ya kifamilia, Mosses Kitandu, Athanas Mdamu na Michael Bosco.

"Uongozi kwa jumla unawashukuru kwa namna walivyoshiriki kuhakikisha timu inabaki Ligi Kuu na unawatakia kila la kheri katika maisha yao ya mpira wa miguu nje ya Prisons," ilisema taarifa hiyo.

## Harmoboy Tz amtamani Ney wa Mitego

**Na Sabato Kasika**

RAPA chipukizi Harmoboy Tz (Maneno Paschal) amesema anatamani kufanya kazi na Ney wa Mitego (Emanuel Elibariki) na wasanii wengine, kwa madai kwamba wanaweza kumsaidia kupiga hatua kutoka sehemu moja kwenda nyingine katika mafanikio.

"Mimi bado kijana, ninapambania ndoto zangu za kuwa msanii mkubwa kwenye muziki wa kizazi kipya, hivyo ni muhimu nitafute sapoti kutoka kwa wakongwe wakiwamo akina Ney," alisema Harmoboy Tz.

Msanii huyo ambaye anatoka mkoani Geita, amesema kwa sasa yupo jijini Dar es Salaam akijaribu kuendelea kipaji chake akiwa ameshafyatua nyimbo kadhaa.

"Kuna nyimbo kama Tunaishi nao na Wamepagawa ambazo zinapatikana katika chaneli yangu ya youtube inayoitwa Harmoboy Tz, mashabiki wa muziki wa kizazi kipya wanaweza kuingia huko,"amesema Harmoboy Tz.

## ZISIKUPITE

### CHELSEA KUMKOSA KOUNDE

MPANGO wa Chelsea wa kumsajili beki wa kati wa Sevilla, Jules Kounde unaelekea kugonga mwamba, huku Barcelona wakizidi kuwa na matumaini kwamba wanaweza kumpata mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 23. ***(The Guradian)***

### TORRES AWINDWA

KAMA Jules Kounde hatajiunga na Chelsea, wataangalia mchezaji wa kimataifa wa Villarreal na Hispania, Pau Torres mwenye umri wa miaka 25, beki wa kati wa Inter Milan na Slovakia, Milan Skriniar mwenye miaka 27 na Mkroatia Josko Gvardiol mwenye miaka 20, ambaye yuko RB Leipzig. ***(90min)***

### WERNER KUWA CHAMBO

KLABU ya Chelsea itamtoa mshambuliaji wa Ujerumani, Timo Werner mwenye umri wa miaka 26 kwa RB Leipzig ili kuishinda Paris St-Germain kwenye mbio za kumsajili mlinzi wa Ufaransa ,Nordi Mukiele mwenye umri wa miaka 24 kutoka klabu hiyo ya Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga. ***(Foot Mercato, kupitia Metro)***

### AZPILICUETA, ALONSO KUZUIWA

CHELSEA itawazuia Barcelona kumnunua mlinzi wa Hispania, Marcos Alonso mwenye umri wa miaka 31 na Cesar Azpilicueta mwenye miaka 32 kutoka kwao, kwa sababu ya kuwazidi kete kwa Jules Kounde. ***(Sport)***

### SCAMACCA HUYO WEST HAM

KLABU ya West Ham imekubaliana na mshambuliaji wa Italia, Gianluca Scamacca na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 na jana Jumanne alitarajiwa kufanyiwa vipimo vya afya yake kabla ya kukamilisha uhamisho wa thamani ya pauni milioni 35.5 kutoka Sassuolo. ***(Mail)***

### KETELAERE OFA MPYA

AC Milan inafikiria kuongeza ofa yao kwa kiungo mshambuliaji wa Club Bruges, Charles de Ketelaere, ambaye amekuwa akihusishwa na Leeds United, ili kufanikisha dili la kumnunua mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji mwenye umri wa miaka 21. ***(Calciomercato)***

### ZIYECH ATAKIWA MILAN

WINGA wa Chelsea, Hakim Ziyech pia analengwa na AC Milan na raia huyo wa Morocco mwenye umri wa miaka 29 anataka kuhamia Serie A. ***(Calciomercato)***

### PAQUETA KUUZWA

KLABU ya Lyon imependekeza kuwa iko tayari kusikiliza ofa kwa kiungo wa kati wa Brazil, Lucas Paqueta mwenye umri wa miaka 24, ambaye amekuwa akihusishwa na Arsenal. ***(Metro)***


### OSIMHEN ANA FURAHA

MSHAMBULIAJI wa Nigeria, Victor Osimhen mwenye umri wa miaka 23 amesema maneno kuhusu mustakabali wake ni "uvumi tu" na "ana furaha sana" kuichezea Napoli. ***(Corriere dello)***

### SESKO NI KOMOA

KLABU ya Red Bull Salzburg imewajibu Manchester United kuhusu kumtaka fowadi wao, Benjamin Sesko mwenye umri wa miaka 19 raia wa Slovenia, kwa kusema wanataka "milioni 300 pamoja na Fernandez Bruno. ***(RB Salzburg kwenye Twitter)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# RONALDO ARUDI MANCHESTER

Ni kwa ajili ya mazungumzo ya mustakabali wake, anataka kucheza timu inayoshiriki Ligi ya Mabingwa Ulaya...

**MANCHESTER, England**

CRISTIANO Ronaldo amesafiri kurejea Manchester kwa mazungumzo kuhusu mustakabali wake huku akipanga kuhama hapo kwenye dimba la Old Trafford.

Ronaldo amekosa maandalizi na United kabla ya msimu mpya, akitaja sababu za kifamilia, na bado hajafanya kazi na kocha mpya Erik ten Hag.

Mshambuliaji huyo wa Ureno aliwasili jijini Manchester Jumatatu na kukutana na United kujadili mustakabali wake.

Kwa mujibu wa 90min, Ronaldo bado ana nia ya kuwaacha Mashetani Wekundu hao na kutaka kwenda kwenye Klabu inayocheza Ligi ya mabingwa Ulaya.

Awali ripoti zilizitaja klabu za Bayern Munich na Chelsea kuwa zinawania saini yake, na sasa Atletico Madrid imetajwa kuwa pia ipo kwenye mpango wa kumchukua.

Ronaldo alikuwa mfungaji bora wa United msimu uliopita akiwa na mabao 24 katika michuano yote huku wakistahimili kampeni mbaya, wakimaliza nafasi ya sita wakiwa na pointi 58 pekee.

Wakati ikibakia kuonekana iwapo Ronaldo ataondoka, mchezaji mmoja ambaye atasalia Old Trafford ni Anthony Martial.

Mfaransa huyo hakuwa na mpangilio mzuri msimu uliopita lakini amemvutia Ten Hag wakati wa mechi za kirafiki za United huko Thailand na Australia.

Martial amefunga mabao matatu katika mechi nne za kujiandaa na msimu mpya, huku United wakipata mabao 13 kwa jumla dhidi ya Liverpool, Melbourne Victory, Crystal Palace na Aston Villa.

Wanamaliza maandalizi yao kwa kucheza dhidi ya Atletico Madrid na Rayo Vallecano kabla ya mechi yao ya kwanza ya Ligi Kuu dhidi ya Brighton.

## HABARI MICHEZO

# LEWANDOWKSI AMKOSHA XAVI



**NEWYORK, Marekani**

ROBERT Lewandowski amekuwa na hisia kali kwa mara ya kwanza akiwa Barcelona, huku kocha, Xavi akimwita "usajili wa ajabu".

Lewandwoski aliichezea klabu yake hiyo kwa mara ya kwanza katika ushindi wao wa 1-0 wa kirafiki dhidi ya Real Madrid Jumamosi, akianza kabla ya kutolewa kipindi cha mapumziko.

Mshindi huyo wa pili wa Ballon d'Or mwaka 2021 anataka kufunga mabao 40 kwa kila msimu kwa misimu saba mfululizo kule Bayern, huku Barcelona wakitumaini kuwa bado yuko kwenye kilele cha uwezo wake licha ya kuwa atafikisha umri wa miaka 34 mwezi ujao.

Akizungumza na vyombo vya habari kuhusu mshambuliaji mpya wa klabu hiyo, Xavi hakuwa na lolote zaidi ya kumsifia.

"(Lewandowski) amezoea vizuri," alisema. "Ni mnyenyekevu sana - ameshinda karibu kila kitu katika ulimwengu wa soka.

"Ana unyenyekevu wa kufanya kazi kwa bidii kwa ajili ya timu, na kwetu sisi ni usajili wa ajabu. Ni mzuri sana, nina furaha sana kuwa na Robert kwenye timu, na (dhidi ya Madrid) alizoea vizuri sana.

"Aliudhibiti mpira wakati Madrid walipokuwa wakipiga juu, alielewa wakati wake wa kudhibiti na kucheza kwa viungo, washambuliaji au kwa kiungo wa ulinzi.

"Aliingia ndani mara nyingi, kwa hivyo tunazungumza juu ya mchezaji bora katika ulimwengu wa soka."

Xavi pia aligusia mkakati wa uhamisho wa Barcelona alipoulizwa kama kuna usajili zaidi uliopangwa, akionesha nia ya kina na ushindani wa kuanza kwa nafasi.

"Naam, zaidi, ni bora," alisema. "Yaani kadiri inavyoweza kushindana ndivyo itakavyotufanya tuwe wafanyakazi, watafanya vizuri zaidi, watashindana wao kwa wao.

"Kuna michezo mingi mwaka huu, ningesema zaidi, kwa sababu kuna Kombe la Dunia na kalenda imebanwa zaidi. Nadhani ni muhimu kuwa na ushindani kati ya wachezaji.

"Kuna majeruhi, kutakuwa na vikwazo - vyema zaidi. Barca, nimeshasema mara nyingi, lazima iwe na wachezaji wawili wa kiwango cha juu katika kila nafasi, na hili ndilo tunalofanyia kazi."

# Juventus yawataka Werner, Martial

**TURIN, Italia**

KLABU ya Juventus inataka kuwasajili, Timo Werner wa Chelsea au Anthony Martial wa Manchester United ikiwa hawataweza kukamilisha dili la kumnunua Alvaro Morata, kwa mujibu wa Sky Sport Italia.

Kocha wa Juve, Max Allegri amemtaja raia huyo wa Hispania kuwa ndiye aliyekosekana ili kukamilisha sura yake mpya akiwa na Dusan Vlahovic na Angel Di Maria.

Morata amerejea Atletico baada ya Juve kushindwa chaguo lao la pauni milioni 29.7 la kumsajili kabisa wakati mkopo wake wa miaka miwili ulipokamilika Juni, kwani walitaka ada ya chini.

Martial alikuwa tayari amevutiwa na Juventus katika dirisha la usajili la Januari kabla ya kujiunga na Sevilla kwa mkopo.

Sky Germany inaelewa kuwa Werner anavutiwa na klabu yake ya zamani ya RB Leipzig, ambayo ilipokea pauni milioni 49 kwa ajili yake wakati kipengele chake cha kuachiliwa kilipofikiwa na Chelsea miaka miwili iliyopita.

Wakati huo huo, Paul Pogba amepata majeraha ya nyama za paja katika mazoezi wiki mbili tu baada ya kurejea Juventus.

Jeraha hilo litamlazimisha kutocheza michezo yote iliyosalia ya Juve ya kujiandaa na msimu mpya na kuna uwezekano akakosa mechi yao ya kwanza ya Serie A dhidi ya Sassuolo Agosti 15 mwaka huu.




BREAKING NEWS

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,018,1

JACKPOT MECHI WIKI HII

TAREHE: 28 JULAI 2022

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 28/07/22 | 19:00 | Paide Linnameeskond vs Ararat Armenia | 2.82 | 3.22 | 2.47 |
| 02. 28/07/22 | 19:30 | El Gouna vs Ismaily SC | 3.06 | 2.96 | 2.44 |
| 03. 28/07/22 | 19:30 | Farco FC vs Talaea El Gaish | 2.86 | 2.61 | 2.91 |
| 04. 28/07/22 | 19:45 | Maccabi Netanya vs Basaksehir | 3.02 | 3.22 | 2.33 |
| 05. 28/07/22 | 19:45 | Elfsborg vs Molde | 2.45 | 3.33 | 2.77 |
| 06. 28/07/22 | 20:00 | Dinamo Batumi vs Lech Poznan | 2.37 | 3.27 | 2.92 |
| 07. 28/07/22 | 20:00 | Olimpija Ljubljana vs Sepsi Osk | 2.52 | 3.19 | 2.78 |
| 08. 28/07/22 | 20:45 | Lechia Gdansk vs Rapid Vienna | 2.54 | 3.30 | 2.69 |
| 09. 28/07/22 | 21:00 | Hamrun Spartans vs Velez Mostar | 2.64 | 3.20 | 2.64 |
| 10. 28/07/22 | 21:00 | FC Vaduz vs Luka Koper | 2.58 | 3.24 | 2.68 |
| 11. 28/07/22 | 21:30 | Buducnost vs Breidablik | 2.39 | 3.44 | 2.78 |
| 12. 28/07/22 | 22:00 | Puskas Akademia vs Vitoria Guimaraes | 2.98 | 3.28 | 2.33 |
| 13. 28/07/22 | 22:00 | Coca Cola vs Zamalek | 3.05 | 3.05 | 2.38 |

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money ZANTEL EZYPESA

SEND

SportPesa

SPORTPESA.CO.TZ

PIGA *150*87#

GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

16,895/-

SUPA JACKPOT

MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 30/07/22 | 17:00 | Cardiff vs Norwich City | 3.09 | 3.29 | 2.29 |
| 02. 30/07/22 | 17:00 | Millwall vs Stoke City | 2.26 | 3.34 | 3.09 |
| 03. 30/07/22 | 17:00 | Rotherham vs Swansea | 2.94 | 3.43 | 2.31 |
| 04. 30/07/22 | 17:00 | Wigan vs Preston | 2.40 | 3.19 | 2.99 |
| 05. 30/07/22 | 17:00 | Bristol Rovers vs Forest Green | 2.33 | 3.33 | 2.98 |
| 06. 30/07/22 | 17:00 | Carlisle vs Crawley Town | 2.27 | 3.28 | 3.13 |
| 07. 30/07/22 | 17:00 | Kilmarnock vs Dundee Utd | 2.26 | 3.24 | 3.19 |
| 08. 30/07/22 | 17:00 | St. Johnstone vs Hibernian | 2.98 | 3.08 | 2.47 |
| 09. 30/07/22 | 17:00 | Morecambe vs Shrewsbury | 2.94 | 3.29 | 2.38 |
| 10. 30/07/22 | 18:30 | GIF Sundsvall vs Varbergs Bois | 2.70 | 3.40 | 2.50 |
| 11. 30/07/22 | 19:00 | Odd Ballklubb vs Rosenborg | 3.03 | 3.38 | 2.28 |
| 12. 30/07/22 | 19:00 | Liverpool vs Manchester City | 2.62 | 3.18 | 2.45 |
| 13. 30/07/22 | 19:15 | Oostende vs Mechelen | 2.70 | 3.45 | 2.48 |
| 14. 30/07/22 | 19:30 | Enppi Club vs Al Masry Club | 3.02 | 2.98 | 2.48 |
| 15. 30/07/22 | 20:00 | Nimes vs Caen | 2.71 | 3.22 | 2.66 |
| 16. 30/07/22 | 20:00 | Le Havre vs Grenoble Foot | 2.33 | 3.08 | 3.33 |
| 17. 30/07/22 | 20:00 | US Quevilly Rouen vs Rodez Aveyron | 2.62 | 3.07 | 2.87 |

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATANO - 27/07/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1089 | Muktijoddha Sangsad KC vs Abahani Ltd. Chittagong | 4.81 | 4.03 | 1.55 |
| 13:00 | 2504 | Busan I Park vs Gwangju | 4.03 | 3.54 | 1.76 |
| 13:20 | 5908 | Japan vs South Korea | 2.05 | 3.19 | 3.34 |
| 13:30 | 3841 | Eastern Suburbs vs Moreton Bay Utd | 2.65 | 3.83 | 2.16 |
| 15:15 | 2864 | Sarawak vs Johor Darul Takzim | 14.66 | 7.04 | 1.12 |
| 15:15 | 3004 | Pahang FA vs Selangor FC | 2.51 | 3.44 | 2.44 |
| 16:00 | 1477 | Kuala Lumpur vs Kedah | 2.26 | 3.09 | 2.99 |
| 16:00 | 2107 | Piteaa IF vs Vasalunds IF | 4.41 | 4.31 | 1.56 |
| 16:00 | 2852 | NoSta vs Dinamo Barnaul | 2.14 | 3.25 | 3.30 |
| 16:00 | 3113 | Negeri Sembilan vs Terengganu | 2.80 | 3.34 | 2.26 |
| 16:00 | 5571 | Orenburg 2 vs Irtysh | 4.31 | 3.73 | 1.67 |
| 17:00 | 1166 | Lech II Pozna vs Pogon Siedlce | 2.15 | 3.15 | 3.15 |
| 18:00 | 1004 | Rosenborg BK 2 vs Rana FK | 1.47 | 4.71 | 4.81 |
| 18:00 | 4042 | Inter Club De Escaldes vs CFR Cluj | 12.13 | 5.66 | 1.23 |
| 18:00 | 5825 | Wigry Suwalki vs KKS 1925 Kalisz | 9.23 | 5.10 | 1.26 |
| 19:00 | 1194 | Pepo Lappeenranta vs MP Mikkeli | 2.71 | 3.25 | 2.36 |
| 19:00 | 1586 | Bodo Glimt vs Linfield Belfast | 1.08 | 8.42 | 27.05 |
| 19:00 | 2207 | Sindri vs KFS | 1.51 | 5.10 | 4.12 |
| 19:00 | 2274 | Vifk Vaasa vs JBK Pietarsaari | 1.75 | 4.02 | 3.58 |
| 19:00 | 4321 | Radunia Stezyca vs Wisla Pulawy | 1.86 | 3.43 | 3.68 |
| 19:00 | 5220 | GKS Jastrzebie Zdroj vs Sokol Ostroda | 1.37 | 4.63 | 6.50 |
| 19:30 | 1374 | Smouha Club vs Arab Contractors | 2.29 | 2.97 | 3.32 |
| 19:30 | 3874 | Pyramids vs National Bank | 1.60 | 3.52 | 6.04 |
| 20:00 | 1874 | Sandefjord vs Kristiansund | 2.12 | 3.48 | 3.17 |
| 20:00 | 2560 | Fredrikstad vs Raufoss | 1.86 | 3.73 | 3.39 |
| 20:00 | 2693 | AIK Football vs Vorskla Poltava | 1.55 | 4.05 | 5.66 |
| 20:00 | 2887 | FC Zurich vs Karabakh | 2.11 | 3.60 | 3.05 |
| 20:00 | 3790 | Malmo vs Zalgiris | 1.20 | 5.81 | 13.03 |
| 20:00 | 5243 | Fenerbahce vs Dynamo Kiev | 1.77 | 3.55 | 4.30 |
| 20:30 | 4563 | Chojnice vs KS Hutnik Krakow Ssa | 1.22 | 5.87 | 8.99 |
| 21:00 | 1006 | RB Salzburg vs Liverpool | 4.51 | 4.02 | 1.59 |
| 21:00 | 1501 | UMF Grindavik vs Thor Akureyri | 1.93 | 3.78 | 3.14 |
| 21:00 | 1728 | Villa Dalmine vs Quilmes | 2.95 | 2.85 | 2.44 |
| 21:00 | 1778 | Temperley vs Atletico Alvarado | 1.93 | 2.99 | 4.02 |
| 21:00 | 1905 | Gimnasia Jujuy vs Nueva Chicago | 2.05 | 2.96 | 3.65 |
| 21:00 | 2139 | Deportivo Riestra vs Ferro CO | 2.60 | 2.90 | 2.70 |
| 21:00 | 2742 | Flandria vs Club Almagro | 2.70 | 2.79 | 2.70 |
| 21:00 | 3598 | Univ San Martin vs Ayacucho | 3.54 | 3.34 | 1.93 |
| 21:00 | 4204 | Gomel vs Aris Salonica | 9.09 | 5.05 | 1.31 |
| 21:00 | 5787 | KI Klaksvik vs Sutjeska | 1.63 | 3.73 | 5.25 |
| 21:05 | 4459 | Gimnasia Mendoza vs Instituto Cordoba | 2.02 | 2.85 | 3.93 |
| 21:30 | 1815 | San Telmo vs Agropecuario | 3.44 | 2.90 | 2.15 |
| 21:30 | 2791 | Slovan Bratislava vs Ferencvaros TC | 2.90 | 3.35 | 2.29 |
| 22:00 | 3089 | Misr Lel Makasa vs Al Ahly Cairo | 13.08 | 5.43 | 1.23 |
| 22:00 | 5343 | Olympiakos vs Maccabi Haifa | 1.70 | 3.56 | 4.71 |
| 22:00 | 5588 | Germany W vs France W | 2.47 | 3.01 | 2.76 |
| 22:15 | 1708 | IR Reykjavik vs Throttur Reykjavik | 2.65 | 3.73 | 2.20 |
| 22:15 | 2309 | Aegir vs Reynir Sandgerdi | 1.41 | 4.82 | 5.51 |
| 22:15 | 5856 | HK Kopavogs vs Grotta | 1.64 | 4.32 | 3.88 |
| 23:00 | 2520 | IF Vestri vs Throttur Vogum | 1.33 | 5.11 | 6.68 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# NYOTA 16 WA TAIFA QUEENS WAITWA KAMBINI

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa Chama cha Netiboli Tanzania (Chaneta) umetaja kikosi cha wachezaji 16 wa timu ya taifa (Taifa Queens) ambao wataingia kambini kuanzia kesho kwa ajili ya kujiandaa na michuano ya kufuzu Kombe la Dunia litakalofanyika kuanzia Agosti 20 hadi 28 mwaka huu nchini Afrika Kusini.

Wakifuzu watakwenda kushiriki michuano ya kombe la Dunia itakayofanyika Oktoba 2023 nchini humo.

Akitaja kikosi hicho jana, Kocha mkuu wa Taifa Queens, Hafidh Tindwa alisema kikosi ambacho wamekichagua wana uhakika nacho na kudai anaamini kitakwenda kuiwakilisha vizuri Tanzania.

"Kikosi ambacho tumekitaja tunaamini kitafanya vizuri na tumechagua kutokana na vigezo vyao kupitia mashindano mbalimbali waliyoshiriki," alisema Tindwa.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa chama hicho, Devota Marwa alisema ifikapo Julai 30 mwaka huu wachezaji wote wanatakiwa wawe wameripoti kambini.

Mwenyekiti huyo alisema licha ya kutaja kikosi hicho vile vile watafanya mchujo baadae ili wapate wachezaji 12 ambao ndio watapata nafasi ya kwenda kushiriki michuano hiyo.

Kikosi ambacho kimetajwa ni pamoja na Penina Lushinge (JKT Mbweni), Siwa Juma Ally (Zanzibar), Doritha Mbunda (JKT Mbweni), Merry Ciana Mashauri (Tamisemi) na Tupegele Lazaro Anyingisye (Zanzibar).

Wengine ni Monica Mdoe (Nyika), Faraja Malaki (Nyika), Gloria Benjamin Mussa (Tamisemi), Zam Zam Mohamed (JKT Mbweni), Sophie Adam Komba (Tamisemi), Jenipher Saningo (Arusha), Dawa Haji Vuai (Zanzibar), Juliana Mwita Mhono (Zanzibar), Lilian Jovin Ndenzako (Tamisemi), Mwanaidi Hassan Ngubege (JKT Mbweni) na Mainda Rogers Gift( Zanzibar).



Nyota wa Timu ya Azam FC, Bruce Kangwa (kushoto), akichuana na Iddy Nado wakati wa mazoezi ya timu hiyo kwenye mji wa El Gouna nchini Misri, jana. Azam imeweka kambi nchini humo kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania bara na michuano ya kimataifa. **PICHA: AZAM FC**

# Mwenyekiti, Katibu wa Njorefa wafungiwa

**Na Shufaa Lyimo**

MWENYEKITI wa Chama cha Soka Mkoa wa Njombe (Njorefa), Tobias Lingala pamoja na Katibu Mkuu, Obed Mwakasungura wamefungiwa kwa muda wa miaka miwili kutojihusisha na masuala yoyote ya mpira wa miguu ndani ya nje ya nchi kutokana na kutokidhi vigezo vya uongozi.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Msajili wa Vyama vya Michezo Tanzania, Riziki Majala alisema adhabu hiyo imetokana na viongozi hao kushindwa kuthibitisha kuwa na elimu ya sekondari ya kidato cha nne na cha sita, ikiwa ni matakwa ya katiba ya chama hicho.

Msajili huyo alisema toleo la sasa ibara ya 29(2) na 29(7) vimetolewa vigezo kuhusu sifa za kuwa wagombea au viongozi wa nafasi hizo.

"Adhabu hizo zimetolewa kwa mujibu wa kifungu cha sheria cha 28 cha Baraza la Michezo Tanzania (BMT) sura ya 49 kikisomwa na kanuni ya 10(1) 10 (1) C, ambayo ipo kwenye kanuni za usajili wa vyama vya michezo ndani ya tangazo la serikali namba 441 ya mwaka 1999," alisema Msajili huyo.

Alisema adhabu hiyo ilianza tangu Julai 20 mwaka huu na kudai watuhumiwa hao wanaruhusiwa kukata rufani ambazo zitapitia kwa Waziri mwenye dhamana ya Michezo, Mohamed Mchangerwa.

Aliongeza kuwa adhabu hizo zimetolewa baada ya kupitia malalamiko mbalimbali ambapo alifanya uchunguzi na kubaini ukweli hivyo kuamua kuwafungia.

***

Mwishe

Michezo
Jumatano Julai 27, 2022
Nipashe



UKURASA 21

Ronaldo arudi Manchester



Wachezaji wa Simba wakijifua kwenye mazoezi jana.**PICHA:SIMBA FC**

# SIMBA SC KARATA YA TATU MISRI LEO

● ● ●Inaivaa El Hodoud ikikumbuka mechi ya mwaka 2010, wawili wapya kutangazwa...

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Simba ambacho kimeweka kambi nchini Misri kwenye jiji la Ismailia, leo kitacheza mechi yake ya tatu ya kirafiki dhidi ya El Hodoud ya huko.

Klabu hiyo imethibitisha kuwepo kwa mchezo huo kwenye mtandao wake wa Instagram ikisema kuwa mechi hiyo itapigwa kwenye jiji la Cairo nchini humo.

Itakuwa ni mechi ya tatu ya kirafiki kwa timu hiyo ambayo inaelekea wiki ya tatu ikiwa tayari imeshacheza dhidi ya Ismailia, ikitoka sare ya bao 1-1, bao la Simba likifungwa na mchezaji wao mpya, Augustine Okra, na ya pili ilikuwa dhidi ya Abou Hamad, ikashinda mabao 6-0, mawili yakifungwa na Pape Sakho akitokea benchini, Erasto Nyoni, Moses Phiri, Meddie Kagere na Jonas Mkude. Mechi hiyo itakumbushia mwaka 2010 timu hizo zilipokutana kwenye Kombe la Shirikisho Barani Afrika, ikiwa ni raundi ya pili. Mechi ya kwanza ikifanyika Aprili 25, kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Simba ilishinda mabao 2-1, lakini ikaenda kubugizwa mabao 5-1, Mei 8 na kutolewa kwenye michuano hiyo.

Wakati huo huo, klabu hiyo imesema bado kuna wachezaji wawili ambao inakamilisha usajili wao.

Meneja Habari na Mawasiliano, Ahmed Ally amesema kuwa mchezaji mmoja amekamilisha kila kitu, lakini anakamilisha taratibu za usafiri, huku mmoja akiwa na matatizo kidogo kwenye usajili wake.

"Mmoja tayari tumemalizana naye, tutamtangaza siku yoyote kwa sababu alichobakisha ni kuwasili tu nchini Misri, ila mmoja bado ana matatizo kidogo na tunaendelea kulitatua," alisema.

Taarifa za ndani zinasema kuwa mchezaji ambaye huenda akatangazwa ni Nelson Okwa kutoka Rivers ya Nigeria, huku mwenye matatizo kwenye usajili wake ni Cesar Manzoki ambaye klabu yake ya Vipers ya Uganda imemuwekea ngumu, akiwa amebakisha mkataba wa miezi miwili tu.

Inadaiwa kuwa klabu yake inataka Simba itoe zaidi ya Sh. milioni 400 ili iweze kuvunja mkataba huo, kitu ambacho kimeleta sintofahamu.

Habari zinasema baadhi ya viongozi wa Simba wapo nchini Uganda kurekebisha mambo, lakini kama ikishindikana basi atasajiliwa kipindi cha dirisha dogo Desemba mwaka huu wakati akiwa mchezaji huru.

## Mkataba wa Nabi Yanga upo, yajifua dakika 300

**Na Saada Akida**

WAKATI programu ya Kocha wa Yanga, Nesreddine Nabi, kucheza mechi za kirafiki itaanza wiki ijayo, huku timu hiyo ikijifua saa tano kwa siku sawa na dakika 300, mazungumzo yanaendelea kuhusu mkataba wake mpya na kila kitu kitawekwa wazi muda si mrefu kwa muda gani ambao ameongeza.

Kikosi cha Yanga kilianza mazoezi rasmi wiki iliyopita kwa kufanya mazoezi mara moja ya uwanjani na sasa wanafanya mazoezi mara mbili kwa siku asubuhi na jioni.

Asubuhi wanafanya saa mbili na jioni saa tatu na kutimiza jumla ya saa tano sawa na dakika 300 kwa siku.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nabi alisema kwa sasa wanaendelea kufanya mazoezi ya Gym kwa ajili ya viungo ambayo yanafanyika asubuhi na jioni uwanjani kwa ajili ya kuweka fiti wachezaji wake.

Alisema ameridhishwa na maendeleo ya kikosi chake na kutarajia makubwa zaidi kwa sababu wachezaji hao wamerejea wakiwa vizuri katika suala la utimamu wa mwili.

Ofisa habari wa klabu hiyo, Hassan Bumbuli alisema wachezaji wa kigeni wawili, Bernard Morrison na Yannick Bangala wameingia jana na leo watangana na wenzao mazoezini kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya.

"Wachezaji wote (wazawa) ambao hawako katika majukumu ya timu ya Taifa, wako kambini na wakigeni kasoro hao wawili ambao wanarejea leo (jana) na kesho (leo) wataingia kambini kuanza rasmi msimu mpya wa ligi," alisema Bumbuli.

Alisema kuhusu mkataba wa kocha wa Nabi, mazungumzo yanaendelea na wiki ijayo kila kitu kitawekwa wazi ikiwemo ni muda gani wa mkataba ambao ameongeza.

"Kikubwa ni kwamba Nabi amethibitisha kuendelea na Yanga na sasa yuko katika maandalizi ya msimu mpya nadhani juu ya mkataba wake tutaweka wazi hili linafanyika sambamba na suala la Yacouba Sogne juu ya makubaliano yetu kwa sababu tayari amemaliza mkataba," alisema Bumbuli.

Alisema ndani ya wiki hii watakuwa na jambo lao ikiwemo kumtangaza rasmi mdhamini wao Mkuu ambaye ameweka mamilioni ya fedha katika klabu hiyo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >